# USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA FILAMU ZA KIBONGO:

# MIFANO KUTOKA FILAMU TEULE ZA STEVEN KANUMBA


Na

Evangelina Rugamba



Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2015

## ITHIBATI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa "**Usawiri wa Mwanamke katika Filamu za Kibongo: Mifano kutoka Filamu Teule za Steven Kanumba"** na anapendekeza ikubalike kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri ya Sayansi za Jamii katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo kikuu cha Dodoma.

…………………………………………….

Prof. Frowin Paul Nyoni

(Msimamizi)

Tarehe………………………

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, Evangelina Rugamba, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia; na kwamba, haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

Saini………………………………

Tarehe………………………………

©Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya Tasnifu hii kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Kazi hii imekamilika kutokana na michango ya watu mbalimbali walionisaidia. Sina budi kutoa shukrani zangu za upendo kwa watu hao. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii kwa kunipa nguvu, maarifa, afya njema mpaka kufanikisha kazi hii.

Pili, ningependa kumshukuru msimamizi wangu, Profesa Frowin Paul Nyoni, ambaye amekuwa nami bega kwa bega katika kutoa mwongozo na mapendekezo kadha wa kadha na kuhakikisha kuwa kazi hii inafanyika katika kiwango hiki.

Tatu, shukrani zangu ziwaendee wahadhiri wangu waalionifundisha kozi za shahada za umahiri. Hawa ni: Daktari Elias M .Songoyi, Profesa Joshua Madumulla, Daktari Athumani Ponera, Daktari Seif Khatibu, na Daktari Rafiki Sebonde. Pia, ninawashukuru wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili, niwataje wachache wafuatao: David Bwandilo, Mhagama Kwame, Mlelwa Anna, Kakuru Yovin, Athumani Ally, Kihaya Duru na Suzana Selemani. Ninawashukuru kwa michango yao mpaka kufanikisha kazi hii.

Nne, napenda kumshukuru mama mzazi Clezensia Kagulaza pamoja na walezi wangu Angelo Rugamba, Daktari Willison Rugamba, kwa kunilea na kunipatia elimu mpaka kunifikisha hapa. Nawaombea kwa mungu awape maisha marefu na baraka tele.

Mwisho, nawashukuru rafiki zangu na wafanyakazi wenzangu walimu wa shule ya Sekondari Katuma ambao ni: Frank Sheshe, Chesco Komba na Lyidia Msigwa .

## TABARUKU

Kwa marehemu baba yangu, Reuben Rugamba na babu yangu Emmanuel Rugamba, hii ni tunu maalumu kwa changamoto zilizowasibu katika uhai wenu ili kunitafutia elimu.

# IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo kwa kujiegemeza katika filamu teule za Steven Kanumba. Nadharia ya Ufeministi ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data wa tasnifu hii. Data zilikusanywa ni pamoja na filamu teule mbili za Steven Kanumba. Filamu hizo zilitazamwa na kuchambuliwa ili kupata umaizi wa usawiri wa mwanamke. Vilevile, makala, vitabu na tasnifu mbalimbali vilisomwa ili kuona ni kwa namna gani mwanamke amesawiriwa.

Utafiti huu umebaini kuwa katika filamu za Kibongo, mwanamke amesawiriwa kwa namna mbalimbali kama vile mama, mtoto, kijakazi, mwalimu, mzimu pamoja na kahaba. Vile vile, utafiti huu umebaini kuwa jamii inamchukulia mwanamke katika mtazamo hasi. Mtazamo huo wa jamii juu ya mwanamke ni pamoja na vipigo na manyanyaso, kiumbe cha kustarehesha ulimwengu, malaya na muasi wa maadili, kiumbe dhaifu pamoja na kuzalishwa na kutelekezwa.

Utafiti huu umebainisha dhamira mbalimbali zilizojitokeza kuhusu usawiri wa mwanamke dhamira hizo zimejitokeza katika pande mbili. Kwa upande wa kwanza dhamira hizo zimejitokeza katika hali chanya kama vile ujasiri na uvumilivu malezi, usiri na staha kwa mwanamke pamoja na misimamo katika maisha. Pia utafiti huu umebinisha dhamira zinazomsawiri mwanamke katika hali hasi kama vile ukatili, unafiki na usaliti, utovu wa maadili pamoja na ushirikina. Aidha, utafiti huu umebaini kuwa adui wa mwanamke ni mwanamke mwenyewe.

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | | |
|---|---|---|
| UKIMWI | = | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| TV | = | Televisheni |
| TGNP | = | Tanzania Gender Networking Programme (Mtandao wa Jinsia Tanzania) |
| TUKI | = | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| VVU | = | Virusi Vya Ukimwi |
| UDOM | = | University of Dodoma |
| UDSM | = | University of Dar-es Salaam |
| ITV | = | Independent Television |

## YALIYOMO

ITHIBATI .................................................................................................... i
IKIRARI NA HAKIMILIKI .................................................................................... ii
SHUKRANI .................................................................................................. iii
TABARUKU .................................................................................................. iv
IKISIRI........................................................................................................ v
VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........................................................................... vi
YALIYOMO .................................................................................................. vii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ..................................................................... 1
1.1 Ufafanuzi wa Istilahi ..................................................................................... 1
1.1.1 Filamu ..................................................................................................... 1
1.1.2 Filamu za Kibongo ..................................................................................... 1
1.1.3 Usawiri wa Mwanamke................................................................................. 2
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ................................................................................ 3
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ............................................................................... 4
1.3 Malengo ya Utafiti ......................................................................................... 5
1.3.1 Lengo Kuu................................................................................................ 5
1.3.2 Malengo Mahususi ...................................................................................... 5
1.4 Maswali ya Utafiti.......................................................................................... 6
1.5 Umuhimu wa Utafiti ....................................................................................... 6
1.6 Mipaka ya Utafiti .......................................................................................... 6
1.7 Nadharia ya Utafiti......................................................................................... 7
1.8 Maelezo Mafupi Kuhusu Steven Kanumba .......................................................... 10
1.9 Hitimisho................................................................................................... 11

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO**.......................................................... 12
2.1 Utangulizi .................................................................................................. 12
2.2 Historia na Maendeleo ya Filamu Nchini Tanzania............................................... 12
2.3 Maandiko kuhusu Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi kwa Ujumla ............. 15
2.4 Maandiko kuhusu Filamu kwa Ujumla ............................................................... 19
2.5 Mapengo Yaliyojitokeza .................................................................................. 24

2.6 Hitimisho ........................................................................................ 25

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI........................................................... 26**
3.1 Utangulizi ........................................................................................ 26
3.2 Usanifu wa Utafiti ........................................................................................ 26
3.2 Eneo la Utafiti ........................................................................................ 26
3.4 Walengwa wa Utafiti ........................................................................................ 27
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa ........................................................................................ 27
3.4.2 Usampulishaji na Sampuli ........................................................................................ 27
3.5 Ukusanyaji Data ........................................................................................ 28
3.5.1 Zana na Njia za Kukusanyia Data ........................................................................................ 28
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Udhibiti wake ........................................................................................ 29
3.6 Uchambuzi na Uunganishaji wa Data ........................................................................................ 29
3.7 Vikwazo vya Utafiti ........................................................................................ 30
7.8 Hitimisho ........................................................................................ 30

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI** 31
4.1 Utangulizi ........................................................................................ 31
4.2 Namna Mbalimbali za Usawiri wa Mwanamke katika Filamu Teule za Steven Kanumba. ........................................................................................ 31
4.2.1 Muhtasari wa Filamu Teule ........................................................................................ 31
4.2.1.1 Muhtasari wa Filamu Teule ya *Fake Smile* (2008) ........................................................................................ 31
4.2.1.2 Muhtasari wa Filamu ya *White Maria* (2010) ........................................................................................ 32
4.2.2 Usawiri wa Mwanamke katika Filamu Teule ........................................................................................ 34
4.2.2.1 Mwanamke kama Mama ........................................................................................ 35
4.2.2.2 Mwanamke kama Mtoto ........................................................................................ 35
4.2. 2.3 Mwanamke kama Kijakazi ........................................................................................ 36
4.2.2.4 Mwanamke kama Daktari na Mwalimu ........................................................................................ 37
4.2.2.5 Mwanamke kama Mzimu ........................................................................................ 38
4.2. 2.6 Mwanamke kama Mwajiri ........................................................................................ 38
4.2. 2.7 Mwanamke kama Kahaba ........................................................................................ 39
4.3 Mtazamo wa Jamii juu ya Mwanamke kupitia Filamu Teule ........................................................................................ 39
4.3.1 Kitega Uchumi ........................................................................................ 40

4.3.2 Vipigo na Manyanyaso ........................................................................... 41
4.3.3 Kuzalishwa na Kutelekezwa ......................................................................... 43
4.3.4 Kiumbe Dhaifu............................................................................................... 44
4.3.5 Malaya na Muasi wa Maadili ........................................................................ 46
4.3.6 Kiumbe cha Kustarehesha Ulimwengu .......................................................... 47
4.4 Dhamira Zinazohusu Mwanamke Katika Filamu Teule ..................................... 49
4.4.1 Dhamira Zinazomsawiri Mwanamke katika Hali Chanya ................................ 50
4.4.1.1 Uvumilivu na Ujasiri..................................................................................... 50
4.4.1.2 Misimamo katika Maisha .............................................................................. 51
4 .4.1.3 Staha na Usiri .............................................................................................. 52
4.4.1.4 Uadilifu na Uchamungu ................................................................................ 53
4.4.1.5 Malezi........................................................................................................... 54
4.4.1.6 Huruma na Utu ............................................................................................. 55
4.4 .2 Dhamira Zinazomsawiri Mwanamke Katika Hali Hasi .................................. 56
4.4.2.1 Unafiki na Usaliti ......................................................................................... 56
4.4.2.2 Utovu wa Maadili.......................................................................................... 58
4.4.2.3 Ushirikina na Uganga.................................................................................... 59
4.4.2.4 Ukatili na Mauaji........................................................................................... 60
4.4.2.5 Umaskini ...................................................................................................... 61
4.5 Hitimisho.......................................................................................................... 62

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .......... 63
5.1 Utangulizi.......................................................................................................... 63
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ...................................................................... 63
5.3 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika ................................................................ 65
5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti..................................................................... 66
5.4.1 Mapendekezo kwa BASATA............................................................................ 66
5.3.2 Mapendekezo Kwa Mtandao wa Jinsia Tanzania ............................................ 67
5.3.3 Mapendekezo kwa Wanawake......................................................................... 67
5.3.4 Mapendekezo kwa Watafiti ............................................................................. 68
5.6 Hitimisho.......................................................................................................... 68
MAREJELEO ....................................................................................................... 69

VIAMBATISHO........................................................................................................ 74
A: Hojaji Iliyotumika Kukusanyia Data ..................................................................... 74
B:  Picha Mbalimbali Zinazohusiana na Tasnifu ....................................................... 75

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Ufafanuzi wa Istilahi

Kwa kuwa kazi hii inahusiana na usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo, zipo dhana za msingi ambazo zinahitaji kufafanuliwa na kutolewa maana ili kuwezesha kuelewa dhana nzima ya filamu na usawiri wa mwanamke kwa ujumla. Istilahi hizo za msingi zilizotumika katika kazi hii ni kama ifuatavyo:

#### 1.1.1 Filamu

Filamu ni sehemu ya fasihi inayoingia katika utanzu wa drama. Neno filamu huhusishwa na neno sinema ambalo nalo linatokana na Kiyunani '*kinein'* lenye maana inayokaribiana na neno la Kiswahili 'kusogea' "wazo la kusogea au kujongea" ndilo lilileta neno la Kiingereza' Movie' ambalo pia humaanisha picha jongefu (Kawini,1992). Hivyo basi filamu ni hadithi yoyote ile inayotambwa kutoka kwa waongozaji wake kupitia picha jongefu zilizorekodiwa kutoka kwenye mazingira fulani, zikiwahusisha waigizaji kutoka kwenye jamii inayoendana na mazingira yao, desturi zao, pamoja na utamaduni uendao sambamba na mawasilisho ya maudhui yaliyosanwa kwenye filamu hizo (Kasiga, 2013).

#### 1.1.2 Filamu za Kibongo

Dhana hii ilitumika kutolea ufafanuzi filamu za video zinazotengenezwa nchini Tanzania. Filamu hizi hutumia muda mfupi katika utayarishaji wake. Lengo kuu la filamu hizi ni kupata soko la kibiashara la ndani na pia kuuza katika nchi jirani za Afrika Mashariki na kati. Nyoni (2013) anafafanua kuwa filamu za Kibongo zenye mrengo wa kibiashara hutawaliwa na mambo kadhaa ikiwemo uwepo wa bajeti finyu pamoja na watayarishaji wasio na ubobevu kwenye utayarishaji wa filamu. Kujivika

fani nyingi wakati wa utayarishaji wa filamu. Matumizi ya mandhari finyu wakati wa utayarishaji, jina la filamu kutumia lugha ya kiingereza. Vilevile, hutawaliwa zaidi na dhamira za mapenzi, uchawi na dini pamoja matumizi ya vitu vya kifahari wakati wa utayarishaji wake kama majumba mazuri, magari ya kifahari na vitu vingine vya kifahari ambavyo haviendani na uhalisia wamaisha halisi ya Kitanzania.

### 1.1.3 Usawiri wa Mwanamke

Ni namna ambavyo mwanamke huchorwa katika kazi za kifasihi. Kwa mfano, mpole, mvumilivu, malaya, mshauri na msiri. Mara nyingi katika kazi mbalimbali za fasihi mwanamke amekuwa akioneshwa katika sura ambayo si nzuri. Tangu jadi taswira ya mwanamke imegawanyika katika sehemu mbili, kwa upande mmoja amekuwa akisawiriwa kama mpole, mvumilivu, mwenye huruma na mnyenyekevu. Taswira hii ndiyo inayokubaliwa kuwa nzuri miongoni mwa jamii mbalimbalili ulimwenguni. Hii ni kwa sababu haipingani na taratibu nyingi za jamii. Kwa upande mwingine, mwanamke amesawiriwa kama kiumbe laghai, mwovu, mzinifu na kigeugeu (Momanyi, 2003). Anaendelea kueleza kuwa wahakiki wengi ulimwenguni wanapoichambua fasihi, picha inayojitokeza zaidi kati ya hizo mbili ni ile ya uovu wa mwanamke. Baadhi ya wasanii wa fasihi wamekuwa wakimchora mwanamke kama chombo cha starehe asiye na uaminifu pamoja na kivutio cha kumfanya msomaji au mtazamaji avutiwe na kazi hiyo. Kwa mfano katika bendi za dansi mwanamke amekuwa akitumika kama kivutio cha watazamaji kwa kuvaa nguo zinazoacha sehemu kubwa ya mwili wake wazi huku akicheza mbele ya hadhira ili kuvutia watazamaji.

Kwa upande wa tamthilia, Penina Mhando ameandika tamthilia nyingi zilizomchora mwanamke kwa namna tofauti tofauti lakini akiwa katika harakati za kujikomboa.

Mfano ni tamthilia ya *Nguzo Mama* (1982) ambayo inamchora mwanamke anavyotaka kujikomboa lakini anashindwa kufanya hivyo kwa sababu ya kukosa msaada kutoka kwa mwanaume. Tamthilia hiyo ya *Nguzo Mama* imeleta mwanga wa kuona kwamba kumbe mwanamke hata katika tamthilia anachorwa kama mtu anayetaka kujikomboa kutoka katika vifungo vya kunyanyasika, kuonewa na kufanya kazi ambazo hazina mshahara.

**1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Sera ya utamaduni ya mwaka 1997 kuhusiana na vyombo vya habari na kazi za kisanaa kama ngoma na filamu inasisitiza uzingativu wa maadili, mila na desturi za Kitanzania katika kuonesha na kurusha vipindi. Hivyo, sheria hii inasisitiza kwamba, sanaa kama muziki, ngoma za asili, filamu na vipindi mbalimbali vinavyodumisha utamaduni vipewe kipaumbele katika kuoneshwa kwenye vyombo vya habari ili kufikisha ujumbe wenye manufaa kwa jamii. Katika kutekeleza dhima hii, ipo bodi ya ukaguzi wa filamu ambayo inaangalia viwango na uhalali wa kuoneshwa kwa filamu hizo kwa kuzingatia maadili na utamaduni wa Mtanzania. Juhudi za kuwa na sheria na hatimaye bodi yenye jukumu la kuhakikisha kuwa maadili hayakiukwi na wasanii inaonesha msisitizo na haja ya serikali na jamii kutunza utamaduni na maadili ya Mtanzania. Kutokana na msisitizo huo, kazi za sanaa zinapaswa kuwasilisha na kuonesha masuala mbalimbali yanayolenga jamii kwa manufaa ya jamii hiyo.

Kama zilivyo kazi nyingine za kifasihi, filamu ni sanaa yenye dhima ya kuakisi masuala mbalimbali ya kijamii. Sanaa ya filamu nchini Tanzania ilianza kushamiri kati ya miaka ya 1990 na 2000. Miaka ya nyuma fani kama filamu na muziki wa bongo fleva hazikuwa mashuhuri katika Tanzania kwa sababu baada ya uhuru na

wakati wa utekelezaji wa Sera ya Ujamaa na Kujitegemea vyombo vya habari vilikuwa chini ya udhibiti wa Serikali (Omari 2009:1). Kushamiri kwa wasanii hasa katika masuala ya muziki na uigizaji wa filamu, kulianza miaka ya 1990. Hali hii ilichochewa na kuanzishwa kwa vituo vya runinga hapa Tanzania miaka ya 1990 na kuwepo kwa mfumo wa soko huria. Kutokana na mfumo wa soko huria, kumekuwepo na uzalishaji wa filamu kiholela ambazo hazifuati vigezo vya utayarishaji wa filamu kimataifa, ambapo kwa mwezi mmoja takribani filamu 20 huzalishwa na kuingizwa sokoni (Kasiga 2013). Hata hivyo kuongezeka kwa filamu kumefungua milango ya ajira kwa watanzania hususani vijana ambao wengi wao wamejiingiza katika utayarishaji wa filamu.

Wasanii mbalimbali wa filamu kama vile Jacob Steven, Vicent Kigosi na Steven Kanumba katika kazi zao wamekuwa wakimchora mwanamke katika mitindo tofauti tofauti lengo likiwa ni kupata soko kibiashara pamoja nakutoa burudani na mafunzo kwa jamii. Hivyo basi, utafiti huu ulijielekeza katika kuchunguza usawiri wamwanamke katika filamu za Kibongo kwa kuzamia zaidi katika filamu za Steven Kanumba ambazo ni *Fake Smile* (2008) na *White Maria* (2010).

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Tasnia ya filamu imeshamiri nchini Tanzania. Sanaa hii yaweza kuwa chombo muhimu katika kufikisha ujumbe na kuisaidia jamii iweze kujitazama na kujikosoa. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa sanaa hii katika jamii, ni watafiti wachache tu ambao wamechunguza sanaa hii hapa Tanzania. Na wengi wao wamejikita katika vipengele vingine kama vile maedeleo ya filamu nchini Tanzania (Mponguliana, 1982), filamu inavyoweza kusadia vijana katika kupambana na unyannyasaji kijinsia (Shule, 2004), Mwelekeo wa utayarishaji wa filamu nchini Tanzania (Kanga’nga

2007), matumizi ya maleba katika filamu za Kitanzania (Gumbo 2010), mwelekeo mpya wa utayarishaji wa filamu nchini Tanzania (Nyoni 2013) pamoja matumizi ya lugha katika kusawiri ujinsia katika filamu za Steven Kanumba (Sued 2013). Vilevile, wataalamu wengi wa kazi za fasihi ambao wamefanya tafiti zao juu ya usawiri wa mwanamke wamejikita katika vipengele mbalimbali vya fasihi kama riwaya, tamthiliya, ushairi, methali na ngano. Mfano Balisidya (1982) ameshughulikia taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi kwa kuzamia katika hadithi fupi na Lyatuu (2011) alichunguza ulinganifu wa usawiri wa mwanamke katika riwaya za waandishi wa kike na riwaya za waandishi wa kiume. Hata hivyo ni watafiti wachache ambao wamefanya tafiti zao kuhusu filamu za Kibongo ambazo nyingi hutayarishwa bila maandalizi ya kutosha kwa ajili ya kupata faida kibiashara. Hivyo basi, utafiti huu uliona kuwa iko haja kubwa ya kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo. Utafiti huu ulijikita zaidi katika filamu za Steven Kanumba ambazo ni *Fake Smile* (2009) na *White Maria* (2010) kwa kuchunguza ni kwa jinsi gani mwanamke amesaweriwa katika filamu hizo.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo ya namna mbili, lengo la jumla na malengo mahususi. Malengo hayo yalituongoza katika kufikia hitimisho la utafiti huu.

#### 1.3.1 Lengo Kuu

Ni kubainisha usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

#### 1.3.2 Malengo Mahususi

a) Kubainisha namna mbalimbali za usawiri wa mwanamke katika filamu teule;

b) Kuchunguza mtazamo wa jamii juu ya mwanamke kupitia filamu teule;

c) Kuchambua dhamira zinazohusu mwanamke katika filamu teule.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

a) Ni namna zipi za usawiri wa mwanamke katika filamu teule?

b) Kupitia filamu teule, je jamii ina mtazamo gani juu ya mwanamke?

c) Ni dhamira zipi zinazojitokeza kuhusu mwanamke katika filamu teule?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kazi yoyote ile ya fasihi ubeba ujumbe ndani yake. Hata kama ujumbe huo haujaelezwa kinagauabaga lakini bado ubaki kuwa ujumbe. Filamu kama kazi ya kifasihi kwa vyovyote vile imesheheni ujumbe uliokusudiwa kufikishwa kwa jamii. Mosi, inatarajiwa kuwa kazi hii itawasaidia watafiti wengine kutafiti zaidi juu ya filamu hasa katika vipengele vingine ambavyo havijaguswa kwa undani kama vile migogoro, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na falsafa za watunzi wa filamu.

Kwa kufanya hivyo, uwanja mpana utaachwa kwa watafiti wengine kutafiti kiundani na kuandika vitabu ikiwezekana. Hili litasaidia kuwa na maejeleo mengi. Pili, utafiti huu utachangia katika kujenga maarifa juu ya fasihi na kuonesha uhusiano uliopo na unaopaswa kuwepo kati ya fasihi na jamii.Tatu, utafiti huu umesaidia kutambua mchango wa tasnia ya filamu katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili.

### 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kipengele kimojawapo cha fasihi ambacho ni filamu kwa kuchunguza filamu mbili za msanii Steven Kanumba ambazo ni *Fake Smile* (2008) na *White Maria* (2010). Tanzu nyingine za fasihi kama riwaya, tamthiliya na ushairi tulizitumia pale ilipobidi katika kushadidia data za utafiti wetu. Aidha, utafiti huu

ulijikita katika kipengele cha maudhui kwa kuchambua nafasi ya mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

### 1.7 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ufeministi au nadharia ya Mtazamo kike. Ufeministi ni mfumo wa mawazo yanayofasiri na yanayoelezea mambo yanayohusiana na uhusiano wa kijinsia na kuwepo kwa mwanamke. Fellenger (1998) anaeleza kwamba nadharia ya Ufeministi inatafuta kuondoa nadharia za utawala wa mwanaume ili kuweka bayana dosari za asili na upofu wa jinsia. Mafeministi wanaendeleza mikabala mipya kutoa fasili ya mwanamke na ukweli kuhusu mwanamke. Tsikataa (1991) anafafanua zaidi kwamba, Ufeministi ni utambuzi wa ubaguzi wa kimfumo dhidi ya wanawake katika uwanja wa jinsia na katika kujitoa kufanya kazi kuyakabili mabadiliko yaliyopo katika jamii. Anazidi kueleza kwamba, baada ya wanawake kuona kwamba wamewekwa katika daraja la mwisho kwenye ngazi zote za maaamuzi kama vile siasa, uchumi na katika ngazi ya jamii, ndipo walipoamua kupambana ili waweze kujikomboa wenyewe. Mwanzoni mapambano hayo yalipigwa vita, lakini kuanzia miaka ya 1800 mpaka 1900 madai yao kama vile haki ya kupiga kura, na kupata nafasi katika ngazi ya uchumi na jamii yalipitishwa. Walionekana wana haki kubwa ya kushiriki katika kuzalisha maarifa kama walivyo na haki ya kuwa sehemu ya maarifa hayo. Nadharia ya Ufeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1790 huko Ulaya. Wanazuoni wa mtazamo kike duniani wamegawa vipindi vitatu katika vuguvugu hili la ufeministi huku kila kipindi kikishughulikia mambo mahususi. (Humm, 1995). Kipindi cha kwanza kilishughulikia vuguvugu katika karne ya kumi na tisa na mwanzoni mwa karne ya ishirini huko Uingereza na Marekani. Kipindi hicho cha kwanza cha vuguvugu la mtazamo kike kilipigania

haki sawa ikiwemo haki ya kupiga kura, kuwa na haki ya kumiliki mali, pamoja na kuwa na haki ya watoto na fedha. Kipaumbele kilikuwa ni kupigania haki za kijamii, utamaduni na usawa wa kisiasa, na hasa haki ya kupiga kura kwa wanawake. Harakati hizi zilisaidia baadaye wanawake kuruhusiwa kupiga kura katika nchi mbalimbali kama vile New Zealand (1893), Norway (1913), Udenishi na Ireland (1915); Umoja wa Kisovieti (1917), Austria, Ujerumani, Poland, Uswidi na Kanada (1918); Uholanzi (1919), Afrika Kusini (1930) na Ufaransa (1945).

Kipindi cha pili cha vuguvugu hili kilipata ushabiki mkubwa na msukumo wa kundi la kiliberali, ki-Marx, kijamaa na siasa kali ya mtazamo-kike katika miaka ya 1960 hadi 1980, na hivyo kusaidia kuimarisha maisha ya wanawake. Matokeo yake, wanawake walilipwa haki sawa na wanaume katika kazi zinazofanana; unyanyasaji wa kijinsia ulififia kazini na wanawake waliajiriwa katika kazi za kitaaluma kama vile sheria na udaktari. Wanawake wengi wakapata nafasi katika vyuo pamoja na kusomeshwa mafunzo yenye mwelekeo wa kijinsia na kadhalika. Nafasi ya kudhibiti miili ya wanawake ikakubaliwa pamoja na kuwa na uzazi wa mpango, utoaji mimba, na wakunga kuruhusiwa kuwaendea wajawazito kuwasaidia. Aidha, vitu vya dharura vya kuwashughulikia wanawake wanaonyanyaswa na wanaume au waume vikawepo ili wanawake na wagonjwa wa akili na wanawake kupata tiba.

Katika kipindi hiki mafanikio kidogo yaliyopatikana yalifaidisha tabaka dogo la wanawake wa tabaka la kati la wanawake weupe tu. Wanawake wengi masikini, weusi, walemavu, na hata wale wasagaji walitengwa kwa tabia zao. Fikira za mawazo ya kipindi hiki cha pili zikapata pingamizi. Ilibainika kuwa jitihada zao haziwakilishi wanawake wa matabaka yote. Wanawake wale waliotengwa kikabila,

kitabaka na jinsia wakatafuta njia zao za kuendeleza vuguvugu lao (Harding, 1991; Hill Collins 1990; Hooks 1989; Smith, 1987).

Kipindi cha tatu kilianza mwaka 1990, huku kikijaribu kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika kipindi cha pili. Lililosisitizwa na kushughulikiwa zaidi ni yapi mambo mema na niyapi mambo mabaya kwa wanawake (Freeman, 2008). Katuli (2002) anaeleza kwamba mafeministi wamegawanyika katika makundi manne ambayo ni Mafeministi wa Kiradikali (wenye siasa kali), Mafeministi wa Kiliberali (wenye kutaka mabadiliko), Mafeministi wa Ki-Marx na Mafeministi wa nchi za dunia ya tatu. Ijapokuwa kila kundi lina msimamo na kanuni zake, lakini lengo la makundi hayo bado ni moja tu la kumkomboa mwanamke.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu. Nchi za Dunia ya Tatu ni kikundi cha nchi zinazoendelea zipatazo 145 zilizopo katika mabara ya Asia na Afrika ambazo ni pamoja na Asia na Afika pamoja na nchi za Afrika mashariki na kati ambazo zinajulikana kwa maisha duni, elimu duni, kipato kidogo cha kujikimu, umaskini na njaa (Mohanty,1991). Nadharia ya Ufeministi katika Dunia ya Tatu pia inajihusisha na ukatili anaofanyiwa mwanamke ikiwa ni pamoja na mila na desturi kama vile ukeketwaji wanawake na kurithi wajane. Wanawake katika nchi za Dunia ya Tatu wanatamani usawa katika jamii, kazini, katika dini na uhusiano binafsi, lakini wanawake hawa wanakumbana na vitisho na ukatili ambao ni mbaya sana.

Nadharia ya Ufeministi ina mizizi katika siasa ya ukombozi. Juhudi ya kuanzisha nadharia hii ilianza katika muungano wa ukombozi wa wanawake uliopamba moto zaidi mnamo miaka ya sitini ikiongozwa na wataalamu kama vile; Semone de Beauviour, Betty Frieden na Kate Millet (Wamitila, 2002). Baadhi ya mambo

yaliyozingatiwa ni kuunda upya uhalisi wa mwanamke kwa kupangua na kudhihirisha miundo ya kijadi ambayo inamtukuza mwanaume na kumkandamiza mwanamke. Mtazamo huu wa kijadi umejengwa kutoka kazi za awali za wanafalsafa ambao kwa umoja wao walionesha kuwa mwanamke si binadamu bora kama alivyo mwanaume. Kwahiyo azma kuu ya hasa ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu ni kusoma upya kazi za fasihi ili kusisitiza umuhimu wa vipengele vilivyopuuzwa na wahakiki wengi au ambavyo hawangeviona kwa sababu walikuwa wanafanya kazi katika nadharia za kijadi zinazomtukuza mwanaume.

Nadharia ya Ufeministi imetumika na imemsaidia mtafiti kuchambua na kuelezea nafasi ya mwanamke katika fasihi. Hivyo nadharia hii ndiyo iliyongoza utafiti huu kwa kuwa inazungumzia masuala yanayohusu wanawake katika Nchi za Dunia ya Tatu na namna ya kutatua matatizo hayo. Pia imetupa mbinu mbadala inayotumika katika kumkuza mhusika wa kike. Hivyo, utafiti huu ni njia mojawapo ya kumnusuru mwanamke na kumpa nyenzo na njia ya kupigana nayo katika Nyanja mbalimbali.

### 1.8 Maelezo Mafupi Kuhusu Steven Kanumba

Steven Kanumba alizaliwa 08/01 /1984 Mkoani Shinyanga nchini Tanzania na alifariki dunia 08/04/2012. Alipata elimu yake ya msingi katika shule ya msingi Buyogi iliyoko Shinyanga na baadaye elimu ya sekondari katika shule ya secondari Mwadui iliyoko mkoani Shinyanga. Baadaye alihamia shule ya sekondari ya Dar es Salaam *Christian Seminary* iliyoko jijini Dar es Salaam. Baada ya kuhitimu kidato cha nne, alijiunga na kidato cha tano katika shule ya secondari ya Jitegemee. Alianza shughuli za sanaa mnamo miaka ya 1990. Mnamo mwaka 2001 alijiunga na kundi la uigizaji la Kaole lililopo jijini Dar es Salaam. Kundi hilo lilikuwa likionesha michezo ya kuigiza kwenye kituo cha runinga cha ITV. Filamu yake ya kwanza iliitwa

*Haviliki* (2005) ambayo ilifuatiwa na filamu ya *Johari* (*2006*) na *Dar 2 Lagos* (2006). Mpaka anafikwa na umauti, Steven Kanumba alikuwa ametoa filamu nyingi zipatazo 30 baadhi ya filamu hizo ni *Fake smile* (2008), *More than Pain* (2010), *Young Billionare* (2010), Uncle JJ (2010), *White Maria* (2010) na *Devil Kingdom* (2011). (http://www.kanumba.com).

### 1.9 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza utangulizi kwa ujumla kuhusu utafiti, Istilahi mbalimbali za utafiti zimefafanuliwa. Aidha, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utatizo za utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti vimejadiliwa. Pia kiunzi cha nadharia kinachoongoza utafiti huu kimebainishwa.Tumeitimisha sura hii kwa kueleza historia fupi ya Steven Kanumba. Sura ya pili inajadili historia ya filamu nchini Tnzania, maandiko kuhusu usawiri wa mwanamke, maandiko kuhusu filamu kwa ujumla, na kuhitimisha na mapengo yaliyojitokeza.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko. Imegawanyika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inafafanua historian a maendeleo ya filamu nchini Tanzania. Sehemu ya pili inafafanua maandiko kuhusu usawiri wa mwanamke katika fasihi kwa ujumla. Sehemu ya tatu inafafanua maandiko kuhusu filamu kwa ujumla. Na sehemu ya tano inaeleza kuhusu mapengo yaliyojitokeza. Mwisho, maelezo mafupi kuhusu sura ya pili pamoja na kudokeza muhutasari wa sura ya tatu.

## 2.2 Historia na Maendeleo ya Filamu Nchini Tanzania

Kwa mujibu wa Nottcut na Lathan (1937), sanaa ya filamu ilianza kuingia nchini Tanzania miaka ya 1920. Kwa upande wa Tanzania maendeleo ya filamu yalichochewa na nchi za Ulaya na za Kiafrika. Mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1920 kulianza kuonekana filamu za Kizungu zilizoletwa na wakoloni kwa lengo la kuimarisha utawala wao katika koloni la Tanganyika. Katika miaka ya 1930 Tanganyika ilichaguliwa Kama kituo cha kimataifa cha filamu kilichokuwa chini ya Wamisheni ambacho kiliitwa BEKE (*Bantu Educational Kinema Experiment*). Utengenezaji wa filamu katika kipindi cha ukoloni nchini Tanzania, unaweza kuangaliwa kuanzia miaka ya 1933 hadi 1960.

Mponguliana (1982) anaeleza kuwa historia ya filamu Tanzania imegawanyika katika vipindi viwili, yaani wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Vipindi hivi vilitofautiana kulingana na matukio yaliyokuwa yakitokea wakati huo. Kwa mfano, filamu zilizoonyesha harakati za kupigania uhuru zilitengenezwa wakati wa

ukoloni.Wakoloni walianza kwa kuingiza filamu kutoka nchini Uingereza ambazo ziliakisi mienendo na utamaduni wa kikoloni. Utengenezaji wa filamu Tanganyika ulianza kati ya miaka ya 1935 na 1936 chini ya kampuni iliyojulikana kama *Bantu Educational Cinema Experiment*. Makao yake makuu yalikuwa Vugiri katika milima ya Usambara, Tanga, ambapo mtunzi alikuwa Notcutt (Gumbo, 2010). Filamu nyingi zilizotengenezwa kipindi hiki zililenga kueneza elimu ya kikoloni na kuimarisha ukoloni.

Mponguliana (keshatajwa) anaeleza kuwa filamu za mwanzo nchini Tanzania zilitumia lugha ya Kiingereza na maneno machache ya Kiswahili, Kisukuma na lugha nyingine za kikabila. Anaendelea kueleza kuwa utengenezaji wa filamu za kifasihi ulianza Tanganyika miaka ya 1950. Filamu hizi zilizingatia vigezo vya kifasihi kama vile fani, maudhui, maana, muktadha wa kifasihi, na matumizi ya lugha yenye mvuto iliyosheheni tamathali za semi. Baadaye, kampuni ya Afrika Kusini ilipewa jukumu la kutengeneza filamu kwa kutumia mandhari na waigizaji wa Tanganyika na kwa lugha ya Kiswahili katika mikoa ya Dar es- salaam na Dodoma.

Wakati wa vuguvugu la kudai uhuru wa Tanganyika (Kabla ya Muungano na Zanzibar), filamu ilikuwa ni chombo cha mawasiliano ya kudai uhuru wa Mtanganyika (kwa wakati huo). Vile vile, filamu zilitayarishwa ili kuweza kuwahamasisha wananchi kubaki vijijini kufanya shughuli za kilimo na kuacha kukimbilia mjini. Katika kipindi hicho, aliyekuja kuwa Waziri Mkuu wa pili wa Tanganyika kwa kati ya miaka ya 1960 na mwanzoni mwa mwaka 1970, Marehemu Rashidi Mfaume Kawawa, aliigiza kama mhusika mkuu wa filamu za *Muhogo Mchungu*, *Chalo Amerudi*, *Juma Matatani* na *Wageni Wema*. (Kang'anga, 2006; Mpongoliana, 1982).

Mponguliana (1982) na Mwakalinga (2003) wanaelezea kuwa katika miaka ya 1960 kulikuwa na jitihada za awali za kufufua tasnia ya filamu nchini Tanzania. Katika kufanikisha hilo mwaka 1963 ilianzishwa Kampuni ya Filamu ya Taifa (NFC) iliyokuwa na jukumu la kusimamia maadili katika utengenezaji wa filamu, na shughuli nzima ya uendeshaji wa filamu nchini Tanzania. Mwaka 1964 wataalamu wa filamu kutoka Yugoslavia walifika Tanzania kupanga upya masuala ya filamu. NFC ilisaidia katika kutengeneza filamu za makala simulizi zilizoelezea mambo halisi kutegemeana na matukio maalumu kama vile ziara za kitaifa, gwaride na shughuli nyingine muhimu.

Baada ya uhuru wa Tanganyika na kufuatiwa na Muungano wa nchi mbili za Tanganyika na Zanzibar, teknolojia ya sanaa ya filamu bado ilionekana kuwa chombo muhimu cha mawasiliano hususani katika kuleta maendeleo kwa taifa la Tanzania. Hivyo basi, mwaka 1968 serikali ya Tanzania, ilianzisha Shirika la Filamu la Taifa (Tanzania Film Company) ambalo lilikuwa limepewa jukumu la kuzipitia na kuingiza filamu nchini, pamoja na kuzitayarisha na kuzionesha. Mwaka 1973, Shirika la Filamu la Tanzania (T.F.C) na ofisi ya Waziri Mkuu walizindua filamu yao ya kwanza iliyoitwa *Fimbo Mnyonge*. Filamu hii ilikuwa imebeba ujumbe unaoendana na sera ya Ujamaa na Kujitegemea iliyokuwa ikisimamiwa kwa wakati huo.

Kutokana na umuhimu mkubwa wa filamu kama sanaa yenye kuwasilisha masuala ya kimaendeleo, mwaka 1974, Taasisi ya Sauti na Picha (Audio Visual Institute) ikaanzishwa ikiwa na lengo la kutayarisha filamu katika mazingira ya Tanzania. Kabla ya kuanzishwa kwa AVI, picha mjongeo zilizopigwa wakati wa uchukuaji picha, ilikuwa ni lazima zipelekwe Uingereza, Afrika Kusini au Yugoslavia ili

ziweze kuhaririwa kuwa filamu ziwezazo kutazamwa. Kwa hivyo kuanzishwa kwa AVI kulikuwa ni tumaini kubwa, kwani taasisi hiyo iliweza kutayarisha habari na makala nyingi za kielimu (Gumbo, 2010).

Kuanzia miaka ya 1990, kumekuwa na kushamiri kwa tasnia ya filamu kutokana na mfumo wa soko huria. Kipindi hiki filamu mbalimbali za ndani na nje ya nchi, michezo ya kuigiza na kazi nyingine zilianza kuoneshwa. Kushamiri huko kwa kazi za sanaa kulitokana na kuanzishwa kwa makampuni na vituo binafsi vya habari kama studio, television,magazeti na redio. Katika miaka ya 1970-1990 palikuwepo na filamu chache za Kitanzania kama vile *Fimbo ya Mnyonge* (1974) *Harusi ya Mariam* (1983) na *Yomba Yomba* (1983). Kushamiri kwa soko la filamu kumeendelea mpaka miaka ya 2000 ambapo soko la filamu limechukua sura mpya na limepiga hatua kwa kuwa na wasanii wengi (Kabore, 2003). Kutazama maendeleo haya ya filamu Tanzania kumetusaidia kuonyesha jinsi tasnia ya filamu ilivyopiga hatua, na kuonesha inakoelekea.

## 2.3 Maandiko kuhusu Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi kwa Ujumla

Nafasi ya mwanamke katika maendeleo ya jamii ni suala ambalo limepata hadhi ulimwenguni kote na ndio maana tumekuwa tukishuhudia wimbi kubwa la malalamiko dhidi ya dhuluma na uvunjaji wa haki za wanawake takribani katika nyanja zote za maisha. Nadharia mbalimbali zenye kushughulikia uhakiki wa masuala ya wanawake katika fasihi zimeibuka kwa lengo la kuangalia nafasi ya mwanamke katika fasihi. Aidha, mikakati mbalimbali imependekezwa kuhusu jinsi mwanamke anavyoweza kushughulikiwa katika fasihi.

Nabahny (1972) katika utendi wa Mwanakupona anasisitiza jinsi ambavyo mwanamke anavyotakiwa kuishi na mumewe kwa maadili mema. Anabainisha kuwa

mwanamke anatakiwa awe mnyenyekevu, mwelevu na msikivu pale mwanamume anaposema au kutoa amri fulani. Utendi huu unatoa mwanga katika kukamilisha utafiti huu hasa katika vipengele vya maadili, utamaduni na dini. Kazi hii kubwa ilitoa mwongozo hasa katika utamaduni na dini, ambazo ni asasi kongwe zilizomuonea, zilizomtweza na kumnyanyasa mwanamke.

Balisidya (1982) anachunguza taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Kitanzania. Katika kazi yake ameangazia hadithi fupi, vitendawili na nyimbo na kubainisha kuwa mwanamke huoneshwa kama mlezi wa familia, chombo cha kumstarehesha mwanaume na kinachomilikiwa na mwanaume. Mtalaamu huyu anaona kuwa mwanamke huwekwa katika nafasi hii kupititia masuala ya utamaduni kama vile unyago. Aidha uzuri anaovikwa ni ule unaomweka katika hali duni. Hivyo basi, kazi ya Balisidya akiwa amejikita katika fasihi simulizi, imetoa mwanga uliosaidia kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu za Ki-Bongo.

Mbughuni (1982) ameandika makala kuhusu taswira ya mwanamke katika riwaya za Tanzania. Anatoa hoja kuwa taswira inayoelezwa kuhusuu mwanamke katika riwaya za Tanzania ni za aina mbili.Ya kwanza ni ile ya Hawa na Biblia ambaye anawakilisha uovu wote katika jamii, mchoyo laghai na shetani.Taswira ya pili inamweka mwanamke jikoni akiwa anatawaliwa na mwanaume. Kazi yake imetusaidia katika utafiti wetu katika kushughulikia usawiri wa mwanamke katika filamu za Ki-Bongo.

Saadawi katika riwaya yake ya *Woman at Point Zero* (1983) aliomchora mwanamke kama jamii ilivyomhesabu. Hata hivyo mwanamke katika riwaya hiyo anaonesha harakati za kujikomboa na kujitoa katika kunyanyaswa, kuonewa na kuwa tegemezi kwa mwanaume, anaondoka na kujitafutia maisha ya uhuru wake yeye mwenyewe.

Kazi hii imesaidia katika tasnifu hii katika kushadidia data za msingi ambazo zilichunguza usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

Senkoro (1987), katika kitabu chake cha fasihi anagusia kwa kifupi uchorwaji wa wahusika katika fasihi ipatikanayo katika mfumo kibepari. Maoni yake ni kwamba katika fasihi inayopatikana katika mfumo huu, mwanamke huoneshwa kama pambo la kutamaniwa na mwanaume au kama kiumbe duni ambaye jukumu lake kuu liko kitandani. Baadhi ya maoni yake aliyotoa yametusaidia katika utafiti huu.

Lughano (1989) amehakiki usawiri wa mwanamke katika riwaya za Euphraise Kezilahabi. Anabaisha kuwa Kezilahabi ni mwandishi ambaye anakatisha tamaa ukombozi wa mwanamke. Maoni ya Lughano ni kwamba, Kezilahabi anaendeleza falsafa ya jamii yake kongwe kuhusu mwanamke, falsafa ambayo inamchukulia mwanamke kuwa kiumbe duni aliye chini ya utawala wa mwanaume. Utafiti huu pia umetusaidia sana katika utafiti wetu kwani maoni yake yameweza kuendeleza mawazo yetu kuhusu usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

Fleming, mwanakatuni wa Uingereza ambaye alianza kuchora katuni kuhusiana na ufeministi mwaka 1978, ananukuliwa na MacCabe (2007), anaeleza kwamba wakati wote wanawake walichorwa vibaya katika vyombo vya habari. Anaongeza kwamba, kwa wanawake hazikuwa habari za kuvutia kabisa kama mwanaume anavyoona vibaya kwa mwanamke kumfanya asiwe na uwezo wa kuzalisha watoto. Anaongeza zaidi kwamba, katuni ni kipazasauti chake katika kuielezea jamii ukweli kupitia picha za kuchora. Maelezo yake yalisaidia mtafiti kuelewa nafasi ya mwanamke na jinsia.

Soko na Senkoro (2009) wameeleza kwa kifupi nafasi ya mwanamke katika fasihi picha ya katuni za michezo. Wanadhihirisha hilo kwa kueleza kwamba nafasi ya

mwanamke katika fasihi picha ya katuni mnato za michezo ni ndogo sana na hata hivyo wamechorwa kikejeli na kwa mabezo. Hawa wamemwangalia mwanamke katika kipengele cha katuni lakini si katika filamu. Hata hivyo makala yao imetoa mchango mkubwa sana katika utafiti huu kwani imetoa mwanga kwa mtafiti kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo.

Khatibu (2010) katika utafiti wake wa Shahada ya Uzamivu anaangalia chanjo za matakwa ya mwanaume katika mwili wa mwanamke kwa kufanya ulinganisho wa ushairi wa Muyaka na Shabani Robert. Khatibu anabainisha kuwa kwa kutumia vichanjio vya kitaswira, zikiwemo sitiari za wanyama, wadudu, mimea, nyota, mwezi na hata lugha ya kawaida, washairi wawili ambao amewatafiti wamemsawiri mwanamke kama chommbo cha kumstarehesha mwanaume. Ijapokuwa kwa kiasi fulani Shabani ameonekana kuwa mtetezi wa mwamke kwa kumpa heshima ya mama. Utafiti wake umetusaidia katika utafiti wetu kuchambua usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

Lyatuu (2011) alichunguza usawiri wa mwanamke kwa kufanya ulinganifu wa riwaya zilizoandikwa na waandishi wanawake ambao ni Balisidya (1981) na Mwanga (1989) na riwaya zilizoandikwa na waandishi wa kiume ambao ni Kezilahabi (1971) na Mohamed (1976). Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa waandishi wa kike wameshiriki pia katika kumsawiri mwanamke katika hali duni na yenye udhalilishaji. Maelezo ya Lyatuu yalitupa picha na sababu nyingine kuwa, kutafuta soko la kazi za fasihi ni miongoni mwa mambo yanayosababisha watunzi hawa kumsawiri mwanamke namna hiyo.

Ligopola (2012) alichunguza nafasi ya mwanamke katika nathari kwa kuzamia zaidi katika nathari za Said Ahmed Mohamed. Katika utafiti wake alibaini kuwa nathari za

Said Ahmed zinamchora mwanamke katika hali halisi kwa jinsi alivyo katika jamii. Ligopola anazidi kueleza kuwa, Said Ahmed hakumchora mwanamke katika mtazamo mmoja. Amemchora katika hali ya kumkweza na wakati mwingine katika hali ya kumbeza lengo lake likiwa ni kumuamsha na kumkomboa. Hivyo basi, kazi ya Ligopola ikiwa imejikita katika fasihi andishi, imetoa mwanga katika utafiti wetu kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

Kimati (2014) alichunguza taswira ya mwanamke katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya kwa kujikita zaidi katika nyimbo za wasanii wa kike. Katika utafiti wake, alibaini kuwa katika tasnia ya muziki wa kizazi kipya wasanii wengi wa kike wanatunga nyimbo ambazo zinamsawiri na kumchora mwanamke kwa namna tofauti. Amebaini kuwa wasanii wengi wa kike wanatoa taswira chanya juu ya mwanamke.

George (2014) anachunguza usawiri wa mwanamke katika tamthiliya teule za mwandishi Penina Muhando. Anabainisha kuwa, katika tamthiliya teule kwa kiasi kikubwa mwanamke anapewa taswira zinazomsawiri katika mtazamo hasi ijapokuwa kuna baadhi ya taswira ambazo zinamtazama mwanamke katika mtazamo chanya. Anafafanua kuwa kwa kiasi kikubwa mwanamke ananyanyaswa na kukandamizwa.

**2.4 Maandiko kuhusu Filamu kwa Ujumla**

Mponguliana (1982) alifuatilia maendeleo ya filamu Tanzania. Alijikita kwenye utengenezaji wa filamu katika kipindi kabla ya ukoloni, baada ya ukoloni na baada ya uhuru. Utafiti uliofanywa na Mponguliana ulitusaidia katika utafiti wetu kwa kuonyesha maendeleo ya sanaa ya filamu nchini Tanzania hususani vipindi mbalimbali ambavyo tasnia hii imepitia. Leveri (1984) katika utafiti wake anaangalia matarajio ya kuwapo kwa soko la filamu nchini Tanzania akizama zaidi katika

kipindi cha miaka kumi ya ufanyaji kazi wa Taasisi ya Sauti na Picha na Shirika la Filamu Tanzania mwaka 1973 – 1983. Katika utafiti wake amejadili kwa kina utendaji kazi wa vitengo hivyo muhimu vya filamu vilivyopata kufanya kazi nchini Tanzania.

Chinyere (1992) anachunguza uchorwaji wa mwanamke katika filamu za video za Ki-Nigeria anazitaja kani zinazowarudisha nyuma wanawake katika kupata maendeleo kuwa ni umaskini, kutokuwa na elimu, dini, utamaduni kandamizi na mfumo dume. Anajikita zaidi katika filamu za Ki-Igbo. Anabainisha kuwa wanawake wanapewa husika zinazowakandamiza. Kazi hii pia ilitoa mwongozo katika utafiti huu kwa kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo.

Mwakalinga (2003) amezungumzia nafasi ya mwanamke katika filamu za Kitanzania. Anaeleza kwamba wanawake wanastahili kusawiriwa katika mtazamo chanya ili kuwasilisha picha sahihi ya wanawake wa Kiafrika. Wanawake pia wanatakiwa kuandika hadithi zao wenyewe, na kutengeneza na kusimamia filamu zao wenyewe. Utafiti wa Mwakalinga umesaidia kuonyesha jinsi ambavyo filamu za Kitanzania zimekuwa zikisawiri wanawake.

Shule (2004) anaonesha jinsi filamu zinavyoweza kusaidia kuwaelimisha vijana wa kiume katika kuzuia unyanyasaji wa kijinsia ambao ni mojawapo ya mambo yanayoweza kusababisha kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI. Kazi hii imetoa mwanga juu ya mambo au majanga ya jamii yanavyoweza kuingizwa kwenye filamu na kutumika kama njia ya kuifundisha au kuikanya jamii.

Kang'anga (2007) anafafanua mwelekeo mpya wa utayarishaji wa filamu nchini Tanzania, kwa kujielekeza zaidi katika changamoto na matarajio ya baadaye ya utayarishaji wa filamu nchini Tanzania. Anazifafanua njia madhubuti zenye

kusukuma misingi imara yenye kuleta maendeleo ya soko la utayarishaji filamu nchini Tanzania. Hoja zake zimetufaa katika utafiti wetu, kwani zimetusaidia kufahamu mwelekeo mpya wa wa utarishaji wa filamu.

Njewele (2007) yeye ametazama jinsi maonyesho ya kitamaduni yanavyotumiwa kwenye filamu za Kiafrika. Anaona kwamba filamu chache sana zinaonyesha maonyesho ya kitamaduni ya Mwafrika. Anataja mifano ya filamu hizo kama *Harusi ya Mariamu* (1985) na *Maangamizi* (1998). Anapendekeza kuwa watengenezaji wa filamu wazingatie maonyesho ya kitamaduni ya Kiafrika katika filamu zao ili kuyahifadhi kwa ajili ya utambulisho na manufaa ya kizazi kijacho. Kwa kuzingatia hili, filamu inaweza kuonyesha au kutambulisha taifa fulani kwa kuangalia yale yanayoonyeshwa hasa kwa kuzingatia utamaduni wa jamii husika. Utafiti wa Njewele unasaidia katika utafiti wetu katika kuchambua usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

Mhando (2007) anazungumzia historia ya Tamasha la Filamu la Kimataifa la Zanzibar (ZIFF) akijikita zaidi katika kuchambua historia na muono wa tamasha hilo la filamu. Katika wasilisho lake anasema kuwa nia ya tamasha la filamu ni kuonesha namna biashara ya utayarishaji wa filamu inavyoweza kukuzwa kupitia tamasha na hivyo kunyanyua kiu ya watazamaij kununua filamu. Mhando anasema kupitia nguvu za kitamaduni na kimawasiliano kutoka kwenye filamu, hufanya filamu kuwa sanaa yenye athari kubwa kihistoria. Katika hadhira ya Kitanzania, shani hii ya tamasha hujifunga kwenye kutoa taaluma na pia tamasha ni nafasi ya kuwaweka huru watu kutoka katika masuala yenye kudunisha utu ambayo huonekana kuwa ni mambo yasiyoweza kubadishwa.

Mohammed (2007) anazungumia vibanda vya kuoneshea filamu akimaanisha vijumba vidogo vilivyopo katika mazingira wanayokaa watu wa hali ya chini ambao kupitia vibanda hivyo vya filamu huweza kupata burudani ya kutazama filamu kwa malipo yanayoendana na hali zao za kiuchumi. Katika utafiti wake anaonesha jinsi mabadiliko ya mazingira ya kuoneshea filamu kutoka kwenye nyumba maalum za kuoneshea filamu hadi kwenda kufikia kwenye vijumba vidogo jinsi yalivyozuka. Kazi hii pia imetoa mwanga katika utafiti wetu katika kutambua utazamaji wa filamu jinsi ulivyopiga hatua.

Gumbo (2010) anaangalia matumizi ya maleba katika filamu za Kitanzania anazamia zaidi katika filamu teule za *Oprah* (2008) na *From China with Love* (2009). Anasisitiza kuwa maleba ni sehemu muhimu sana katika utayarishaji wa filamu kwa kuwa huonesha hadhi za wahusika na filamu yenyewe kwa ujumla. Anaeleza zaidi kuwa kutokuwa na elimu ya kutosha katika suala la maleba na ufinyu wa bajeti za kutayarishia filamu ndicho chanzo cha kutokuwa na filamu zilizochaguliwa maleba yenye kuendana na husika zinazoiigizwa na wasanii wa filamu. Kazi hii ilitoa mwanga katika utafiti huu kubainisha usawiri mwanmke katika filamu za Ki-Bongo.

Kisomi (2012) anazungumzia mapambano ya uharamia wa kazi za sanaa ya filamu kupitia chama cha hakimiliki cha Tanzania. Katika Tasnifu yake hiyo ya shahada ya Uzamili katika sanaa za maonesho, anasema licha ya utayarishaji wa filamu nchini Tanzania kupiga hatua nao uharamia wa kazi za wasanii umezidi kushamiri. Katika utafiti wake anaangali changamoto ambazo watayarishaji wa filamu na wasambazaji wa filamu wanazozipata katika upambanaji na uharamia wa kazi za filamu pamoja na kutazama mchango wao katika mapambano dhidi ya uharamia huo wa kazi za sanaa.

Kwenye utafiti wake huo alioufanyia katika Jiji la Dar es Salaam, amegundua kuwa tatizo la uharamia wa kazi za filamu ni kubwa na limewaathiri sana watayarishaji wa filamu. Anasema Katika mapambano ya uharamia wa kazi za filamu, wapambanaji wamekuwa wakikutana na changamoto mbalimbali ikiwemo uwepo mdogo wa nguvu kazi ya kupambana na uharamia, msaada mdogo kutoka polisi na kushindwa kwa watayarishaji kuwa na nguvu moja itakayowawezesha kupambana na uharamia. Mtafiti huyu anashauri ili kuweza kuondoa changamoto hizo serikali inapaswa kuongeza fungu la kifedha, Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) kipatiwe mamlaka ya kuharibu vifaa vyote vinavyotumiwa na maharamia pindi wanapowakamata.

Kasiga (2013) amechunguza U-Nigeria katika utayarishaji wa filamu za Kitanzania, chanzo chake na athari zake kwa Watanzania. Anabainisha kuwa chanzo cha U-Nigeria katika filamu za Kitanzania kuwa ni mwigo wa kiutayarishaji uliotokana na msukumo wa kutafuta soko la ndani kwa watarishaji wa filamu za Kitanzania ambalo lilikuwa limetekwa na filamu za Ki-Nigeria. Aidha athari za U-Nigeria anazigawa kwa namna mbili yaani athari hasi na athari chanya. Kazi hii imetoa mwanga hasa katika utayarishaji wa filamu za Kibongo namna zinavyomsawiri mwanamke.

Sued (2013) amechunguza matumizi ya lugha katika usawiri wa ujinsia katika filamu za Steven Kanumba. Filamu alizochunguza ni *Moses, My Valentine na Johari*. Anabainisha kuwa kuna matumizi ya kejeli na dhihaka zaidi kuliko vipengele vingine vya lugha. Vilevile, anabainisha kuwa katika filamu teule mwanamke amesawiriwa kwa namna inayoonesha tofauti iliopo kati ya mwanamke na mwanaume katika jamii, mwanamke anaonekana dhaifu kuliko mwanaume. Wakati Sued akijifunga kwenye usawiri wa ujinsia kwa kuangazia zaidi matumizi ya lugha,

sisi tumeshughulikia usawiri wa mwanamke katika filamu teule kwa kuzamia zaidi katika kipengele cha maudhui. Hivyo basi, kazi yake imetoa mwanga mkubwa katika kukamilisha utafiti huu.

Nyoni (2015) anabainisha mwelekeo mpya wa utayarishaji wa filamu nchini Tanzania. Anavigawa vipindi vya utayairishaji wa filamu katika matapo matatu tapo la kwanza ni urasimi (*classical period)* tapo la pili ni nyakati za kiza (*dark ages*), tapo la tatu ni kipindi cha mvuvumko (*Renaissance period*). Katika tapo la urasimi anazungumzia uanzishwaji wa filamu nchini Tanzania na jinsi serikali ilivyokuwa muaasisi wa uatayarishaji huo uliozaa filamu kama *Fimbo ya Mnyonge* na *Harusi ya Mariam*. Katika tapo la nyakati za kiza anazungumzia kuanguka kwa utayarishaji wa filamu nchini Tanzania. Kipindi cha mvuvumko anazungumzia utayarishaji wafilamu wa kipindi cha sasa, anafafanua kuwa utayarishaji huu ulishamiri kutokana kuingizwa kwa flamu za nje hasa za Ki-Nigeria pamoja na kukua kwa teknolojia ya utayarishaji wa filamu. Andiko hili pia lilitupatia mwongozo katika utafiti wetu katika kufahamu historia ya utayarishaji wa filamu nchini Tanzania.

## 2.5 Mapengo Yaliyojitokeza

Pamoja na wataalamu mbalimbali wa fasihi kuchambua mambo muhimu juu ya usawiri wa mwanamke na filamu kwa ujumla, bado kazi zao zimeacha mapengo kadhaa nayo ni: Mosi, tafiti zilizochunguza usawiri wa mwanamke katika fasihi nyingi zimejikita katika vipengele vingine vya fasihi kama tamthiliya, riwaya, na ushairi. Pili, tafiti tangulizi kuhusu tasnia ya filamu, nyingi zimejikita katika kuchunguza vipengele vingine katika tasnia hii kama vile maendeleo ya utayarishaji wa filamu na matumizi ya maleba na mapambano ya uharamia katika sanaa ya filamu. Tatu, tafiti zilizofanya uchunguzi kuhusu usawiri wa mwanamke katika

filamu zimejikita katika vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha yanavyomsawiri mwanamke nakuacha vipengele vingine vya maudhui kama vile dhamira. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza utangulizi wa sura ya hii kwa ujumla ambayo imegawanyika katika sehemu nne.  Katika sehemu ya kwanza tumepitia maandiko kuhusu usawiri wa mwanamke katika fasihi kwa ujumla. Sehemu ya pili maandiko kuhusu filamu kwa ujumla yameelezwa Na sehemu ya tatu tumebainisha mapengo yaliyojitokeza, na mwisho tumetoa hitimisho la sura hii. Sura inayofuata ni sura ya tatu ambayo inajadili mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusika na mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumiwa na mtafiti ili kupata data. Pamoja na mbinu ambazo zilitumiwa kuzichambua na kuziwasilisha data hizo kulingana na mada ya utafiti.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu umefanyika maktabani na uwandani. Data zilikusanywa kutokana na maandiko mbalimbali yahusuyo usawiri wa mwanamke, uhakiki wa filamu teule za Steven Kanumba. Pia tulipata nafasi ya kuwahoji watazamaji wa filamu za Kibongo hususani za Steven Kanumba kuhusu usawiri wa mwanamke. Mbinu ya ufafanuzi wa kina na uelekezaji wa jambo kwa kina ndiyo iliyobeba utoaji wa matokeo ya utafiti huu. Data mbalimbali zilizokusanywa zilihakikiwa, kuchambuliwa na hatimaye kufafanuliwa kwa kina.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika mikoa ya Dar es salaam na Dodoma nchini Tanzania. Maeneo haya yaliteuliwa kutokana na sababu zifuatazo. Kwanza, Dar es salaam ilikuwa ni rahisi kupata vyanzo vya kimaktaba vyenye taarifa mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti. Kwa mfano, Taasisi yaTaaluma ya Kiswahili iliyopo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Taasisi ya Taaluma na Maendeleo. Pia ndio mji ambao filamu za Kibongo zinatayarishwa kwa wingi hivyo ilikuwa ni rahisi kupata taarifa zinazohusiana na mada ya utafiti. Mji wa Dodoma ulitumika pia kukusanyia data za uwandani na maktaba. Maktaba ya Chuo Kikuu cha

Dodoma ilitumika kwa kusoma tasnifu, vitabu na makala mbalimbali. Pia ulitumika kuwapata watazamaji wa filamu za Kibongo ambao ni wanafunzi wa vyuo vikuu vya Mtakatifu Yohana cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Dodoma.

## 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa kwa ujumla wake na sampuli inayoshughulikiwa.

### 3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Jamii ya Watafitiwa ni jumla ya vitu vyote ambavyo mtafiti anaweza kuvitumia kwa ajili ya kupata data za utafiti wake (Kasiga, 2013). Huweza kuwa kundi la watu, eneo fulani la kijiografia, aina ya mimea au aina fulani ya maandiko. Jamii iliyolengwa kutoa taarifa za utafiti huu ilijumuisha makundi yafuatayo:

a) Filamu za Kiswahili, hususani za Steven Kanumba;

b) Maandiko mbalimbali kuhusu usawiri wa mwanamke;

c) Watazamaji (20) wa filamu za Steven Kanumba ambao ni wanafunzi wanaosomea shahada ya kwanza katika vyuo vikuu vya Mtakatifu Yohana cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Dodoma.

### 3.4.2 Usampulishaji na Sampuli

Sampuli ni sehemu ya populesheni ambayo mtafiti alitumia katika ukusanyaji wa taarifa zilizosaidia kufikia malengo ya utafiti. Mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji nasibu, lengwa na holela, ambapo kila mhusika anapewa nafasi sawa ya kuchaguliwa na kujumuishwa katika sampuli. Katika utafiti huu mtafiti aliwachagua wawakilishi hao kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya

utafiti bila kuzingatia jinsi zao. Sampuli hiyo ilichaguliwa kiholela kutoka katika makundi yote yaundayo jamii tafitiwa ili kufutoa fursa kwa kila mlengwa kutafitiwa. Sampuli hiyo ilihusisha filamu mbili ambazo ni *Fake Smile* na *White Maria* .Watazamajia wa filamu za Ki-Bongo ambao ni wanafunzi ishirini kutoka vyuo vikuu vya Mtakatifu Yohana cha Tanzania pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma. Walihojiwa ili kupata taarifa zaidi zilizosaidia katika kukamilisha utafiti huu. Mtafiti alitumia filamu za *Fake Smile* na *White Maria.* Sababu hasa ya kuteua filamu hizo ni kutokana na malengo ya tasnifu yenyewe ambapo filamu hizo wahusika wake wakuu ni wanawake vilevile ni filamu ambazo hazijafanyiwa utafiti kuhusu usawiri wa mwanamke.

### 3.5 Ukusanyaji Data

Sehemu hii inaelezea njia na zana mbalimbali zilizotumika kukusanyia data, pamoja na utaratibu kuhusu mchakato wa kukusanyia data.

#### 3.5.1 Zana na Njia za Kukusanyia Data

Zana zilizotumika kukusanyia data za utafiti huu ni hojaji, runinga na deki yake, kalamu za kuandikia, kinyonyeo, ngamizi na mikanda ya filamu za Steven Kanumba pamoja na daftari la kunukuu maelezo. Mbinu nyingine ni miongozo ya kusoma kutoka tasnifu, vitabu na makala mbalimbali kuhusu usawiri wa mwanamke na filamu kwa ujumla. Hivyo njia zilizotajwa zilitumika sambamba na mahojiano, uangaliaji na uhakiki wa filamu zilizoteuliwa na mapitio ya vyanzo mbalimbali vya kimaktaba vinavyohusu taaluma ya filamu na usawiri wa mwanamke.

### 3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Udhibiti wake

Kipindi cha ukusanyaji data, Mtafiti aliomba ridhaa ya watu binafsi ili watafitiwe. Maadili mengine ya utafiti kama vile utunzaji wa siri za taarifa na ufichwaji wa majina ya watoa data yamezingatiwa kwenye utafiti kulingana na matakwa ya watafitiwa. Data za msingi katika tasnifu hii zilipatikana kwa kutazama filamu teule za Steven Kanumba ili kuchunguza usawiri wa mwanamke. Mikanda ya filamu za *Fake Smile* na *White Maria* ilinunuliwa na kutazamwa kupitia runinga ili kupata data za msingi. Data za maktabani zilikusanywa kwa njia ya kudurusu ambapo tulitumia mwongozo wa usomaji katika kusoma tasnifu, vitabu, majarida na vielelezo mbalimbali vya habari kutoka kwenye mitandao. Hojaji ilitumika katika kukusanyia data kutoka kwa watazamaji wa filamu za Steven Kanumba. Daftari, kalamu na ngamizi zilitumika kunukuu data zilizopatikana wakati wa uhakiki wa filamu teule . Vile vile vifaa hivyo vilitumika wakati wa kuchambua na kuunganisha data za utafiti.

## 3.6 Uchambuzi na Uunganishaji wa Data

Uchambuzi wa data za utafiti huu umezingatia nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu. Data zote zilichanganuliwa kwa mkabala usio wa kiidadi, yaani ule wa maelezo. Hii ni kwa sababu utafiti huu sio wa kitakwimu. Data zote zimepewa msimbo ili kuiweka tasnifu katika mtiririko na mpangiziilio mzuri. Data fuatizi zimenukuliwa pale ilipobidi ili kudhibitisha uchambuzi wa data za msingi. Pia data zimepangwa kulingana na malengo ya maswali ya utafiti, hii ni kwa sababu mtafiti alitaka uchanganuzi wa data hizo ulandane na malengo ya utafiti sambamba na kujibu maswali ya utafiti ili kurahisisha zoezi la upangaji kulingana na malengo na maswali. Data zimechanganuliwa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti wetu. Hivyo, kila lengo limeunda sehemu yake katika sura ya nne ambapo kila moja

lina maudhui yake yanayolandana na mada hiyo. Mbinu ya ufafanuzi imetumika katika kuchambua data kwa sababu utafiti huu sio wa kitakwimu. Sehemu kubwa ya data za utafiti huu ni ya maelezo. Data zilizopatikana uwandani kupitia hojaji, utazamaji na uhakiki wa filamu ziliwianishwa pamoja na zile za kimaktaba zilizopatikana kupitia nyaraka mbalimbali ili kupima na kutathimini ubora na udhabiti wake.

### 3.7 Vikwazo vya Utafiti

Mchakato mzima wa utafiti ulikabiliwa na matatizo kadhaa katika hatua zake mbalimbali ulizopitia. Tatizo kubwa lilikuwa ni upungufu wa fedha za kutosha, na muda mfupi ambao mtafiti alitakiwa kuwa amekamilisha utafiti huu. Mtafiti alikabiliana na tatizo hili kwa kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali. Kikwazo kingine kilikuwa ni baadhi ya watafitiwa kutokuwa tayari kutoa taarifa kwa wakati kutokana na kutingwa na shughuli nyingine za kimasomo. Mtafiti alikabiliana na tatizo hili kwa kuomba miadi ya kukutana siku inayofuta.

### 7.8 Hitimisho

Sura hii imeeleza kuhusu mbinu na vifaa vya utafiti vilivyotumika katika utafiti huu. Imeeleza kuhusu mbinu zilizotumika katika kukusanya data, usampulishaji na sampuli. Pia uchanganuzi wa data na udhibiti wake umeelezwa na kumalizia na vikwazo vya utafiti. Sura nayofuata inahusu uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha, na kujadili data kutoka vyanzo mbalimbali. Uwasilishajia wa data kwa mujibu Tromp na Kombo (2006:110) ni namna ya kupangilia data ili ziweze kueleweka vizuri. Uwasilishaji umefanywa kwa mbinu ya ufafanuzi kulingana na malengo mahsusi ya utafiti. Pia nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu imetumika.

## 4.2 Namna Mbalimbali za Usawiri wa Mwanamke katika Filamu Teule za Steven Kanumba.

### 4.2.1 Muhtasari wa Filamu Teule

Katika utafiti wetu filamu zilizofanyiwa uchunguzi ni mbili *Fake Smile* na *White Maria*. Filamu hizo ziliteuliwa kutokana na ukweli kwamba ziliweza kukidhi lengo la utafiti wetu ambalo lilikuwa ni kubainisha usawiri wa mwanamke. Sehemu ifuatayo inatoa muhtasari wa filamu hizo.

#### 4.2.1.1 Muhtasari wa Filamu Teule ya *Fake Smile* (2008)

Filamu ya *Fake Smile* imetayarishwa na Mtitu Game mwaka 2008. Mwandishi wa muswada na mongozaji ni Steven Kanumba. Wahusika katika filamu hii ni: Steven Kanumba, Neshi Adam, Grace Mapunda, na Aunty Ezekiel. Batuli ni msichana mrembo mwenye tabasamu zuri mpole na mnyenyekevu ambaye alilelewa na mzazi mmoja, yaani mama yake, baada ya mama huyo kupata ujauzito akiwa bado mwanafunzi. Kutokana na ujauzito huo, mama Batuli alifukuzwa shule na

kukataliwa na mumewe aitwaye Nashoni ambaye ndiye baba yake Batuli. Baada ya kujifungua mama Batuli alipata bahati ya kuendelea na shule lakini kwa bahati mbaya alipata ujauzito mwingine ambao alipewa na mwanaume mwingine ambaye naye alimtelekeza pamoja na mtoto wake aitwaye Betha. Mama Batuli anakumbana na changamoto ya kulea watoto peke yake bila msaada kutoka kwa baba za watoto hao. Kutokana na hali ngumu ya maisha waliyokuwa nayo familia ya Batuli, binti huyu anaamua kutafuta kazi ili aweze kumsaidia mamayake. Anafanikiwa kupata kazi za ndani kama mtumishi wa nyumbani kwa mama mmoja ambaye anahaidi kumsaidia matatizo yake. Mambo yanakuwa kinyume na matarajio yake baada ya mama huyo kumtumikisha kingono kwa kumuuza kwa wanaume huku akilipwa fedha nyingi wakati Batuli akiambulia ujira kidogo. Kutokana na hali hii Batuli anapata magonjwa ya ngono. Ghafla maisha ya Batuli yanabadilika baada ya kukutana na kijana tajiri aitwaye Bosco ambaye anaamua kumsaidia binti huyu ili hapo baadaye aje kuwa mke wake. Bosco anamjengea nyumba anamnunulia gari, pia anampeleka nje ya nchi kupata matibabu vilevile, anamsomesha hadi ngazi ya elimu ya juu. Batuli akiwa chuoni anabadilika kitabia baada ya kukutana na kijana aitwaye Benjamini. Anaanzisha mahusihano ya kimapenzi na Benjamini bila kujua kuwa Benjamini ana mahusiano ya kimapenzi na binti mwingine aliyekuwa akifanya biashara ya ukahaba. Kutokana na hali hii Batuli anapata maambukizi ya VVU ambayo yanasababisha ugonjwa hatari wa UKIMWI.

#### 4.2.1.2 Muhtasari wa Filamu ya *White Maria* (2010)

Filamu hii imetayarishwa na Mtitu Game mwaka 2010. Mwandishi wa muswada na muongozaji ni Steven Kanumba. Wahusika ni Steven Kanumba, Wema Sepetu, Mayasa Mrisho, Asha Jumbe na Emanuel Myamba. Filamu hii inahusu mabinti

watatu ambao ni Joyce, Patricia pamoja na Maria. Mabinti hawa walipoteza maisha yao kutokana na unyanyasaji wa kijinsia. Hivyo wanaamua kurudi duniani kama mizimu ili walipize visasi kwa wale wote waliosababisha vifo vyao.

Patricia ambaye anatumwa duniani na mkubwa wao aende katika familia ya Prof.Dumba akiwa kama mfanyakazi wa ndani ili alipize kisasi katika familia hiyo kutokana na unyama aliotendewa na mke wa Prof.Dumba. Hapo zamani binti huyo alikuwa akiishi katika familia hiyo akiwa kama mtumishi wa ndani. Prof.Dumba alimshawishi binti huyo na kufanya naye mapenzi kwa bahati mbaya binti huyo alipata ujauzito. Aliishi katika nyumba ya Prof.Dumba mpaka alipofikia wakati wa kujifungua. Siku moja alishikwa na uchungu wa kujifungua akiwa ndani kwa Prof. Dumba. Mke wa Prof.Dumba alitumia mwanya huo kumuua Patricia pamoja na mwanawe aliyekuwa tumboni. Hivyo, Patricia anarudi duniani katika familia hiyo kulipiza kisasi akiwa na sura nyingine tofauti, anaajiriwa kama mtumishi wa ndani, anafanikiwa kulipiza kisasi kwa kumuua mtoto wa Prof.Dumba na kutoweka duniani.

Joyce anakuja duniani katika familia ya mzee Onesmo kulipiza kisasi kutokana na kifo cha mama yake pamoja na yeye mwenyewe. Hapo zamani mama yake Joyce aliyejulikana kwa jina la Anna aliishi katika familia ya mzee Onesmo akiwa kama mtumishi wa kazi. Siku moja mzee Onesmo alimbaka na kumsababishia kupata ujauzito. Anna alipomweleza mzee huyo kuhusu ujauzito, mzee Onesmo alikuja juu kwa kumtukana, kumpiga na kumfukuza. Binti huyo alifariki wakati akijifungua kutokana na kukosa msaada na huduma za kitabibu. Kwa bahati nzuri mtoto wake aliokolewa na msamalia mwema ambaye alimlea, lakini kwa bahati mbaya msamalia huyo alifariki kwa ugonjwa wa kansa wakati Joyce akiwa na umri mdogo. Ndipo

mtoto huyo alipoanza kuzunguka mitaani bila makazi maalumu. Siku moja akiwa katika mizunguko yake ya kutafta chakula majalalani, ghafla alikutana na kundi la vijana watano, waliombaka na na kumpiga na kitu kizito kichwani hadi akapoteza maisha. Hivyo, Joyce amerudi duniani katika familia ya baba yake ambaye ni mzee Onesmo kulipiza kisasi cha mama yake pamoja na yeye mwenyewe anafanikiwa kumuua mtoto wao wa mwaka mmoja kwa kumnyofoa moyo na kupotea nao.

Naye Maria anarudi duniani kulipiza kisasi katika familia ya bwana na bibi Conrad kutokana na unyama aliotendewa na Conrad. Hapo zamani Maria na Conrad walikuwa na mahusiano ya kimapenzi, walipendana sana lakini ghafla penzi lao liliingia dosari pale Maria alipopata ujauzito wa Conrad. Alipomweleza kuhusu hilo, kijana Conrad alikuja juu na kumtaka atoe ujauzito huo kwani yeye hayuko tayari kuitwa baba. Maria hakukubaliana na hilo; ndipo Conrad alipoamua kukodi kundi la vijana pamoja na yeye mwenyewe walimkamata kwa nguvu na kumtoa mimba kwa nguvu. Kutokana na hali hiyo Maria alipoteza damu nyingi na kupoteza maisha. Hivyo, anarudi katika familia hiyo kulipiza kisasi kwa kuwaua watoto wa Conrad na kumshinikiza Conrad akakili makosa yake yote kanisani mbele za watu ndipo atakapomsamehe.

### 4.2.2 Usawiri wa Mwanamke katika Filamu Teule

Katika filamu teule tulizozichunguza mwanamke amesawiriwa kwa namna mbalimbali. Aidha, matokeo kupitia mahojihano na kundi lengwa yanaonesha kuwa katika filamu teule msanii ameonesha namna mbalimbali za usawiri wa mwanamke zenye kuonesha uhalisia wa mwanamke katika jamii. Usawiri wa mwanamke katika filamu teule umeainishwa kama ifuatavyo:

#### 4.2.2.1 Mwanamke kama Mama

Katika filamu teule mwanamke amesawiriwa kama mama yaani mzazi wa kike, mlezi wa familia. Usawiri wa mwanamke kama mama unajidhihirisha kwa kutumia Mama Batuli katika Filamu ya *Fake Smile*. Huyu ni mwanamke ambaye ni mlezi wa familia ya watoto wawili, Batuli na Betha, ambao kila mmoja ana baba yake, na baba wa watoto hawa wamewatelekeza. Mama huyo pamoja na kukumbana na changamoto mbalimbali za kiuchumi, lakini anasimama kidete katika kuwalea watoto wake hadi wanafikia umri wa utu uzima. Bi Catherine pia katika Filamu ya *White Maria* anadhihirisha uhusika wa mwanamke kama mama. Amechorwa kama mama wa nyumbani mlezi wa familia ambaye anajishughulisha na kazi za nyumbani kama vile, kupika, kuosha vyombo, kufua nguo pamoja na kuhakikisha shughuli zote za nyumbani zinaenda sawa. Mafeministi wanafafanua kwamba kazi zilizofanywa na wanawake tangu zilipoonekana kuwa kazi zilifanywa kwa malipo katika nyanja za umma. Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu imeweka nguvu katika kumkomboa mwanamke. Ukombozi huu ni pamoja na suala zima la mgawanyo wa majukumu kijinsia, inataka mwanamke naye afanye kazi zenye tija na manufaa.

#### 4.2.2.2 Mwanamke kama Mtoto

Uhusika wa mwanamke katika filamu teule, amesawiriwa kama mtoto. Aidha usawiri wa mwanamke kama mtoto umengawanyika katika pande mbili. Kwa upande wa kwanza mwanamke amesawiriwa kama mtoto mpole mnyenyekevu mwenye upendo na huruma, kwa kumtumia mhusika Batuli katika filamu ya *Fake Smile*, amechorwa kama mtoto mpole, mwenye adabu na utii ambaye anakutana na matatizo mbalimbali ya kimaisha ambayo yanasababisha binti huyu kupata gonjwa hatari la UKIMWI. Kwa upande mwingine mwanamke amechorwa kama mtoto

mwenye malezi mabaya, asiye na adabu wala utii. Mhusika Betha ni binti aliyewakilisha husika hii kwani ameonekana ni binti mwenye dharau, kiburi na mwenye maneno machafu kwa dada yake pamoja na watu wengine.

#### 4.2. 2.3 Mwanamke kama Kijakazi

Katika filamu teule usawiri wa mwanamke kiuchumi amesawiriwa kama kijakazi yaani mtumishi wa kazi za ndani. Mtunzi amemtumia mhusika Batuli katika filamu ya *Fake Smile* ambaye alikuwa anafanya kazi za ndani kwa Anti ambaye alikuwa anamtumikisha Batuli kwa kumuuza kingono kwa wanaume huku akimlipa ujira kidogo.Vilevile, Joyce na Patricia katika filamu ya *White Maria* ni wasichana ambao wamesawiriwa kama watumishi wa ndani ambapo Patricia aliajiriwa kwa Prof.Dumba na Joyce aliajiriwa kwa Onesmo.

Wasichana hawa wanawakilisha wasichana wengi wanaofanya kazi za ndani ambao katika kukabiliana na maisha wanakumbana na changamoto nyingi ambazo zinasababisha kupoteza maisha au kubeba mimba za utotoni. Patricia na Joyce, wanawakilisha wasichana wanaonyanyaswa kijinsia na kupata misukosuko, wanapokuwa katika harakati za kujikwamua katika ugumu wa maisha. Mafeministi wanafafanua kwamba kazi zilizofanywa na wanawake tangu zilipoonekana kuwa kazi zilifanywa kwa malipo katika nyanja za umma. Mwanzoni wanawake walikuwa wakizaa watoto na kuwalea, kusafisha na kupanga nyumba, kuwatunza na kuwajali wazee na wagonjwa, na kuchangia katika kazi za wanaume lakini bado hazikuhesabiwa kama kazi, na wanawake wote waliofanya kazi hizi waliitwa “mama wa nyumbani”. Ijapokuwa kazi nyingi zimeandikwa kuhusiana na kumtetea mwanamke lakini bado ubaguzi katika kazi za uzalishaji mali katika jamii na familia bado unaendelea.

TGNP (2001) wanasema kwamba wanawake wengi wameajiriwa katika kazi za sulubu zisizohitaji ujuzi au zinazohitaji ujuzi kidogo, zenye fursa ndogo za kujielimisha, kupanda cheo, au kujipatia kipato na maslahi zaidi. Mwanamke anahesabiwa kuwa mama wa nyumbani tu, na kazi zake haziwezi kubadilisha chochote hata kama atazifanya kwa bidii. Kwanza anayezithamini ni yeye mwenyewe, na ni kazi ambazo hazina mshahara. Lakini mwanaume anahesabika kuanzia ngazi ya familia mpaka katika ngazi ya jamii, na kazi zake zinaonekana kuwa ni kazi kwani zinathaminiwa na watu katika jamii, ni kazi zinazoleta mabadiliko. Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu inapigania ukombozi na usawa kwa mwanamke usawa hua ni pamoja na haki ya kuajiriwa. Hivyo, nadharia hii imesaidia kuyaweka wazi matatizo yanayowapata wanawake ili yaweze kutatuliwa. Usawiri wa uhusika wa mwanamke kama kijakazi unasawiri maisha halisi ya wanawake na mateso wayapatayo katika harakati za kujikwamua kiuchumi.

#### 4.2.2.4 Mwanamke kama Daktari na Mwalimu

Katika filamu teule tulizozichunguza, usawiri wa uhusika wa mwanamke katika kujikwamua kiuchumi amesawiriwa kama dakitari na mwalimu. Mwanamke amesawiriwa kama daktari ili kuwakilisha baadhi ya wanawake ambao wamepata elimu na wanajikwamua kiuchumini. Mwanamke daktri anawakilisha madaktari wanaofuata maadili yao ya kazi kwa kutoa ushauri faafu pamoja na kuhudumia wagonjwa kwa wakati. Vilevile, katika filamu ya *Fake Smile* mwanamke amepewa nafasi ya mwalimu yaani anajikomboa katika suala la kiuchumi. Mtunzi ametumia mwalimu wake Grace katika kuonesha hili. Mwanamke huyu anawakilisha baadhi ya wanawake ambao wamepata elimu na kujikomboa kiuchumi. Hivyo, kwa kutumia Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu ambayo inapigania ukombozi wa

mwanamke katika nyanja mbalimbali mojawapo ya malengo yake yameweza kufikiwa kwani mwanamke naye ameweza kufanya kazi za kuajiriwa na zenye tija.

#### 4.2.2.5 Mwanamke kama Mzimu

Mzimu ni kivuli cha mtu aliyekufa zamani, anayemtokea mtu katika ndoto. Katika filamu teule ya *White Maria*, mwanamke amesawiriwa kama mzimu ambao umerudi duniani kulipiza visasi kwa wale wote waliohusika na kifo chake. Katika kudhihirisha hili mtunzi amemtumia Maria Adamu aliyerudi duniani kulipza kisasi katika familia ya bwana Conrad, kutokana kuuwawa wakati akitolewa mimba na bwana huyo. Vilevile, Patricia na Joyce wanarudi duniani kama mizimu kulipa visasi kwa wote waliohusika na vifo vyao.

#### 4.2. 2.6 Mwanamke kama Mwajiri

Katika utafiti wetu tumegundua kuwa mwanamke amepewa nafasi ya tajiri na mwajiri mwenye uwezo wa kimaisha. Aidha, utajiri huo anaupata kwa njia zisizo halali. Mhusika Aunti katika filamu ya *Fake Smile* amesawiriwa kama mwanamke mwajiri wa Batuli ambaye alikuwa anamdhalilisha Batuli kwa kumfanyisha mambo yaliyo kinyume na matakwa yake kwa kutumia kofia ya kumsaidia. Batuli alilazimishwa kushiriki kufanya ngono na wanaume ili aweze kutunza familia yake. Ingawa mwanamke huyu alipewa pesa nyingi, lakini alimlipa Batuli pesa kidogo. Mwanamke ameonekana ni mhusika mkuu katika kuwanyanyasa wanawake wenzake. Ni mtu asiye na huruma na mrudisha nyuma maendeleo ya wanawake wenzake kwa ujuzi wa hali ya juu, kwani ana taaluma hiyo na ni mzoefu wa kuteka wanaume na kuwauza mabinti. Funzo linalopatikana hapa ni kwamba adui wa mwanamke ni mwanamke mwenzake. Hivyo basi, wanawake wanapaswa kupendana

na kuthaminiana. Kwa kufanya hivi tutakuwa tunaenda na malengo ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu.

### 4.2. 2.7 Mwanamke kama Kahaba

Pia mwanamke amesawiriwa kama kahaba ambapo anauza mwili wake ili kujiingizia kipato. Mhusika Samia katika filamu ya *Fake Smile* mpenzi wa Benjamini ndiye hasa mwenye tabia hiyo. Samia ameonekana akijiuza usiku mtaani jijini Dar es Salaam hali iliyosababisha kumwambukiza virusi vya UKIMWI Benjamini.

Pia mwanamke anaonekana kuwa mwili wake ni chombo cha starehe kwa mwanaume. Aidha, mwanamke hujiingiza katika biashara ya ukahaba kutokana na maisha magumu, ukosefu wa elimu pamoja na tamaa ya mali na pesa inamfanya mwanamke kutokuridhika na kile alichonacho, hivyo huufanya mwili wake kama bidhaa ambayo inaweza kubadilishwa na pesa au mali wakati wowote na mahali popote. Usawiri huu wa mwanamke unatoa changamoto kwa wananadaharia ya Ufeministi kumpigania mwanamke katika kupata elimu ili aweze kufanya kazi zenye tija nasio kazi za kumdhalilisha kijinsia.

## 4.3 Mtazamo wa Jamii juu ya Mwanamke kupitia Filamu Teule

Katika kuchambua filamu teule na pia mahojihano na kundi lengwa kupitia, matokeo yanaonesha kuwa jamii inamtazama mwanamke kwa namna mbaliambali . Aidha, utafiti huu umebaini kuwa fikra za jamii kuhusu mwanamke katika filamu teule zinamweka mwanamke katika mtazamo hasi kama kiumbe dhalili na dhaifu. Mtazamo wa jamii juu ya mwanamke umejadiliwa kama ifuatavyo.

### 4.3.1 Kitega Uchumi

Mwanamke ameonekana akitumika kama chombo cha biashara ambapo kazi yake ni kumuingizia kipato tajiri yake kwa kumstarehesha mwanaume. Mhusika Anti katika filamu ya *Fake Smile* ndiye hasa mwenye tabia hiyo ya kuwauza binti wadogo ili wamuingizie kipato. Batuli aliuzwa na mama huyu kwenda kumstarehesha mteja wake, alimfanya kama biashara yake ya kumuingizia kipato kikubwa ili hali Batuli mwenyewe akitaabika na kuambulia magonjwa ya zinaa. Hughes (2000) anasema kwamba ukahaba sio kitu cha asili au kisichokwepeka katika dunia kwa ujumla ila ni udhalilishaji wa wanawake kijinsia. Anazidi kueleza kwamba ukahaba umewafanya wanawake kuwa kama bidhaa na kuwauza kwa mwanaume yeyote anayetaka, na hili linafanywa sana na wanaume watu wazima, wanaume wa makamo na wazee. Hii ni kwa sababu wanaume hao watu wazima wanaona wanaojiingiza kwenye biashara ya ukahaba ni wasichana wadogo ambao wanaume wanasadiki kwamba sio waathirika wa UKIMWI. Lakini hata hivyo bila kujali kujiingiza kwa mabinti wadogo katika ukahaba lakini hawawezi kujitoa kwa sababu kuna wanaume na wanawake ambao wana madanguro yanayowauza mabinti hao. Hapa jamii inapewa changamoto kwa kushindwa kuwapa wanawake nafasi sawa na wanaume katika ajira halali za uzalishaji mali na hivyo kuwaacha wanawake wakijiuza na kuendelea kuwa duni mbele ya wanaume. Mwanamke anaonekana kama kifaa cha kukidhi haja za kingono za mwanaume. Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu inatambua kuwa mwanamke anadhalilika na kunyanyasika. Hivyo kazi ya nadharia ni kujenga sura mpya na kurejesha utu na thamani ya mwanamke na kuondoa dhana potofu zinazoelekezwa kwa mwanamke.

### 4.3.2 Vipigo na Manyanyaso

Suala la vipigo na manyanyaso kwa mwanamke katika jamii limekita mizizi. Katika filamu teule mwanamke anapigwa na kunyanyaswa na mwanaume hususani pale anapodai haki yake. Mhusika Grace katika filamu ya *Fake Smile* ameonekana akipigwa na kunyanyaswa na mpenzi wake Nashoni baada ya kumwambia kuwa ana ujauzito wake na amefukuzwa shule hivyo washirikiane katika kulitatua tatizo hili. Matokeo yake aliambulia matusi na kupigwa. Msanii yeyote yule hufanya sanaa yake kulingana na mazingira yanayomzunguka kama asemavyo Kezilahabi (1983:230) katika Makala ya Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III, anasema kwamba;

> Waandishi wengi waliofanikiwa ni wale waliowaweka wahusika wao chini ya misingi ya mazingira wanayoyaelewa na hasa yale ya kabila lao, ili kuweka hadharani tatizo la kitaifa.

Wanafasihi wanavyomchora mwanamke katika hali ya kunyanyaswa na kuumizwa kila mara hutokana na hali halisi waionayo katika mazingira halisi yanayowazunguka. Na hili linathibitishwa na mafeministi wanaosema kwamba, wanawake wote wanaishi katika hali ya kunyanyasika lakini ni wajibu wa kila anayenyanyasika kujikomboa (York na wenzake, 1991). Changamoto ya ubabe huo inayochukuliwa kama mabavu ya mwanaume ni kitambulisho kinachomuelezea mwanaume.

Hata hivyo, TGNP (2001) wanasema kwamba itikadi ya kawaida inayotumika ulimwenguni kote kuunda mahusiano ya kijamii ni 'mfumo dume' ambao unabainisha dhima duni ya wanawake pamoja na jinsi wanavyonyanyaswa na kunyonywa. Suala la wanawake kufanyiwa vitendo vya kikatili limekita mizizi katika jamii ya Kitanzania. Mfano zipo baadhi ya jamii ambazo huamini kuwa

kumpiga mwanamke ni kumuonesha upendo. Katika filamu ya *White Mria* mwanamke ameonekana akifanyiwa vitendo viovu vyenye kumuumiza mwili wake na hata kumsabishia kupoteza maisha. Mathalani mhusika Joyce alifanyiwa vitendo hivi na Mke wa Onesmo baada ya mama huyo kugundua kuwa, Joyce alikuwa akimtumia mwanae kwenda kuomba pesa mtaani huku akidai kuwa ni mwanae na anaumwa anahitaji kumpeleka hospital. Vilevile, Joyce alipigwa na kundi la vijana baada ya kumbaka mpaka akapoteza maisha. Hii inadhihirisha kwamba katika jamii wanawake wanafanyiwa vitendo vya kikatili ambavyo uwathiri kimwili, kisaikolojia, na kiakili. Vilevile, katika filamu teule mwanamke anatendewa vitendo vya ubakaji. Idadi ya matukio ya ubakaji inayozidi kuongezeka kuripotiwa kwenye vyombo vya habari inadhihirisha wanawake wanavyo nyanyaswa kijinsia ubakaji ulivyo tatizo kubwa katika jamii ya Kitanzania. Matukio hayo yanahusisha watu wazima wanaobaka watoto wadogo, vijana wanaobaka vijana wenzao, watu wazima kubaka watu wazima wenzao, na wanaume wanaobaka vikongwe.

Katika filamu ya *White Maria* vitendo vya ubakaji wanawake vinajitokeza pale Prof.Dumba anapombaka Anna ambaye alikuwa ni mtumishi wake wa ndani, na hatimaye kumpa ujauzito na kumtelekeza. Aidha Joyce nae alibakwa na kundi la vijana wapatao watano wakati alipokuwa akizunguka mitaani kujitaftia chakula,na baada ya kutimiza aja zao walimpiga na kumuua. Matukio ya ubakaji hutokea sehemu nyingi kama sehemu za kazi na waathirika wengi ni wanawake, ambao huishia kupata mimba na maradhi. Aidha, wanawake hawa huwa na nafasi za kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa pamoja na mimba zisizotarajiwa. Matatizo haya ya kubakwa, hutokea wakati wa kutafuta nafasi za ajira, nafasi za masomo au misaada mbalimbali. Pia, upo ubakaji wa vikongwe na watoto wadogo, ambao, huweza kufanyika kwa ajili ya imani za kishirikina. Vilevile, mwanamke

amesawiriwa akifanyiwa vitendo vya kikatili vyenye kumdhalilisha kama vile kutolewa mimba kwa nguvu bila ridhaa yake. Hii inajidhihirisha pale ambapo mpenzi wa Maria anamlazimisha Maria atoe mimba. Maria anaonekana kutokukubaliana na suala hilo. Kitendo cha Maria kugoma kutoa mimba kinamkasirisha mpenzi wake Conrad, ndipo anaamua kufanya njama ya kumtoa mimba kwa nguvu anamua kutafta vijana wanamkamata Maria na kumtoa mimba.Kutokana na hali hii Maria anapoteza damu nyingi na kupoteza maisha. Uamuzi wa Maria kugoma kutoa mimba unaonyesha jinsi alivyokuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na athari za utoaji mimba. Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu inajihusisha nakupinga matendo ya kikatili kama hayo. Hivyo inasisitiza ukombozi wa mwanamke katika nyanza zote likiwemo suala la mahusiano na mapenzi.

### 4.3.3 Kuzalishwa na Kutelekezwa

Msanii amemchora mwanamke katika hali ya umasikini, kula kwa shida, kuvaa kwa shida na anaishi nyumba za kupanga huku akikabiliana na adha za mwenye nyumba. Vilevile, watoto wake wanashindwa kupata elimu. Hali hii imetokana na kuzalishwa na kutelekezwa bila msaada wowote toka kwa baba za watoto hao. Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu inaonesha kuwa moja ya matatizo yanayowakumba wanawake ni pamoja na kunyanyasika katika suala zima la mapenzi. Mtunzi ametumia mhusika Grace katika Filamu ya *Fake Smile* kudhihirisha hili ambapo alitelekezwa na wanaume baada ya kumpa ujauzito huku wakikwepa majukumu muhimu yanayohusu uzazi na ulezi wa watoto. Katika suala la afya, hasa ya uzazi, sehemu kubwa ya wanaume haijihusishi. Hivyo, mwanamke hapati matunzo yanayostahili ili aweze kupata afya, ila anaishi kwa kunyanyasika mpaka

atakapojifungua. Uzazi kama huu ndiyo uliowasababisha mafeministi kutaka mfumo huru wa uzazi uwepo katika jamii. Yaani, watoto wazaliwe kwa kutumia njia za kisayansi. Mwanaume aweke mbegu zake za kiume katika chupa basi huko zirutubishwe na hatimaye mtoto aumbike. Hii ingewafanya wanaume wengi kuwaona wanawake kama watu wenye thamani na bila wao hawawezi kupata raha yamapenzi. Data zinaonesha kuwa katika jamii nyingi hususani vijijini mwanamke hana uwezo wa kumkatalia mwanaume idadi ya watoto anaowataka. Yeye ni kuzaa tu mpaka pale mwanaume atakaporidhika.

Balisidya (1982) anasema kuwa katika jamii zetu, hasa zile za kimaskini, mwanamke anatakiwa kuzaa watoto wengi ambao watamsaidia katika uzalishaji. Na mwanamke asiyezaa hudharauliwa sana na huishi kwa masimango na mateso sana katika familia ya mume wake. Kama kungekuwa na ushirikiano madhubuti kati ya mwanamke na mwanaume huenda mwanaume angeelewa umuhimu wa kupanga uzazi. Malezi na matunzo ya mimba ni muhimu kwani hii itamuepusha mama mjamzito na maradhi madogo madogo ambayo yangeweza kumkuta na kusababisha kifo.

### 4.3.4 Kiumbe Dhaifu

Katika kazi mbalimbali za fasihi kama vile riwaya, tamthiliya na ushairi, mwanamke amekuwa akisawiriwa kama kuimbe dhaifu. Watunzi mbalimbali wa kazi za fasihi wamejaribu kutunga na kusana kazi zao ili kujaribu kuonyesha ni kwa namna gani mwanamke ananyanyasika kijinsia ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo . Baadhi ya waandishi wa tamthiliya wanaogusia suala hilo ni Muhando, katika *Nguzo Mama*, (1982) na *Hatia (*1976). Katika filamu teule tulizozichunguza tumebaini kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe dhaifu kutokana na fikra zinazoelekezwa

kwake. Kuna semi kadha wa kadha ambazo zimeonekana kumdhalilisha mwanamke pamoja na kumdunisha na kuonekana kiumbe dhaifu mbele ya mwanaume. Aidha, utafiti huu umegundua kuwa si mwanaume pekee anayeonekana kumdharau mwanamke, bali mwanamke mwenyewe pia anajidharau nakujiona duni mbele ya mwanaume. Mathalani katika filamu ya *Fake Smile* mwanamke ameonekana kiumbe dhaifu asiye na thamani yoyote katika jamii. Mfano maneno yafuatayo yanaonesha kumdunisha mwanamke "mimi siwezi kuhudumia mijitu ambayo haina faida kwangu"maneno haya aliyasema baba yake Betha akimtukana mama Batuli na wanae baada ya mama Batuli kuomba amsaidie pesa ya matumizi. Hii inaonyesha dharau kwa mwanamke kwa kumwona kama kiumbe ambacho hakina faida katika jamii kwani maneno haya yamemsawiri mwanamke kwa kuashiria dhana hasi kwa mwanamke kwa kumdunisha na kumnyima hadhi ya utu. Mwanamke amechorwa kuwa dhaifu mbele ya mwanaume kwani hawezi kuitetea ndoa yake kwa kumkemea mume, sababu inayowafanya mafeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu kutaka kumkomboa mwanamke. Mafeministi wanadai kwamba ili mwanamke akombolewe kutoka katika udhaifu huo lazima awe thabiti kiasi cha kutosha ili kulazimisha mabadiliko yatokee.

Katika uchunguzi wetu, utafiti umebaini kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe dhaifu asiye na thamani. Mathalani, usemi ufuatao kutoka katika filamu teule ya *White Maria* unaonesha jinsi mwanamke alivyoduni mbele ya mwanaume. Mwanaume anatumia nguvu zake kumnyanyasa kijinsia "sitaki kuharibiwa maisha na kinyago cha kike kama wewe, ulikuja nyumbani kwangu kufanya kazi na sio kuzaa, mbwa wewe ondoka nyumbani kwangu". Maneno haya aliyasema bwana Onesmo akimwambia Anna baada ya kumwambia kuhusu ujauzito wake aliokuwa

nao. Maneno haya yanadhihirisha ni kwa kiasi gani mwanamke hana thamani mbele za mwanaume na ni mtu asiye na faida yoyote katika jamii.

Tunaweza kuyalinganisha maneno haya, na maneno aliyoyasema Bwana Chowe kwenye Tamthiliya ya *Hatia*, iliyoandikwa na Penina Mhando, msanii anasema;

> Bw.Chowe (Anamwigiza) kilio? Labda.
>
> (kwa ghadhabu) Mimi kila siku nawaambia watoto wa kike hovyo sana mnanibishia.

Maneno haya yanadhihirisha ni kwa kiasi gani jamii inamuona mwanamke kama kiumbe asiye na thamani wala faida. Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu inapigania haki na usawa wa mwanamke. Nadharia hii huzamilia kuonesha kwamba uhusiano na usawa kati ya mwanamke na mwanaume ni jambo la msingi. Vilevile, mwanamke amesawiriwa kama mtu mnyonge na dhaifu hii inadhihirika kutokana na fikra zinazoelekezwa dhidi yake katika filamu teule. Mathalani maneno haya yanadhihirisha hilo "usiwe na roho nyepesi kama mwanawake" maneno haya aliyasema sekretari wa Conrad wakati akimsihi Conrad akaze moyo waende kwa mganga wa kienyeji kutafuta dawa ya kumkinga na mzimu wa Maria unaomtokea mara kwa mara. Usemi huu kwa hakika una lengo la kumdunisha mwanamke na kumkweza mwanaume, hali hii inalenga kuaminisha kuwa mwanamke ni mtu dhaifu asiyeweza kuhimili mikimiki ya maisha, hivyo hawezi kusimama mwenyewe mpaka awepo mwanaume.

### 4.3.5 Malaya na Muasi wa Maadili

Dhana ya umalaya na uasi wa maadili kwa mwanamke imejengeka katika fikra za wanadamu toka enzi za Adamu na Eva kuwa mwanamke ndiye chanzo cha mwanadamu kutenda dhambi. Katika filamu teule mwanamke amesawiriwa kama

malaya na muasi wa maadili. Katika filamu ya *Fake smile* suala ya umalaya na uasi wa maadili kwa mwanamke ni suala ambalo limejitokeza kwa kiasi kikubwa. Mathalani mhusika Sania, ndiye aliyekuwa akifanya biashara ya ukahaba katika jiji la Dar -es-salaam, mtunzi ameonesha jinsi alivyokuwa akijihusisha na mapenzi holela na wanaume tofauti tofauti kwa nyakati tofauti, bila kutumia kinga. Biashara hii ya ukahaba ndiyo iliyomsaidia kukidhi mahitaji yake ya kila siku pamoja na kumpatia kula. Kutokana na tabia yake hiyo, alimsababishia mpenzi wake Benjamini kupata maambukizi ya UKIMWI. Vilevile, mwanamke amesawiriwa kama mtu asiye na maadili na anajihusisha na ngono zembe. Kutokana na ngono zembe na ukosefu wa maadili Grace anashindwa kumaliza masomo yake kutokana na kupata ujauzito. Hali hii inasababisha kufukuzwa shule na kushindwa kutimiza ndoto zake. Umalaya na uasi wa maadili umewaweka watu wanawake kwa wanaume katika uwezekano wa kupata maambukizi ya UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa. Wapo wasichana ambao wamelazimika kukubali ngono zembe kutokana na shida mbalimbali za kimaisha. Pia, ukosefu wa huduma muhimu kutoka kwenye familia zao na ukosefu wa elimu ya kutosha juu ya athari ya ngono zembe kumewafanya wasichana kujiingiza katika kufanya ngono zembe. Hivyo basi, ni jukumu la Watanzania kupiga vita umalaya na ngono zembe kwa kuwa waaminifu katika mapenzi,na wasichana wapewe elimu uzazi ili waweze kuepuka mimba zisizotarajiwa.

### 4.3.6 Kiumbe cha Kustarehesha Ulimwengu

Utafiti wetu umebaini kuwepo kwa mtazamo katika jamii kuwa mwanamke ni nyenzo au kifaa cha kustarehesha ulimwengu yaani ni chombo cha starehe na kutoa burudani kwa watu wengine. Kwa mfano katika matangazo mengi ya kibiashara mwanamke hutumika kama kivutio cha kuvuta wateja. Mfano katika matamasha

mbalimbali ya muziki wanawake hutumika kama kivutio cha watazamaji kwa kuvaa nguo zinazoacha sehemu kubwa na miili yao wazi. Mathalani katika filamu ya *Fake smile* mwanamke amesawiriwa kama chombo cha starehe. Kwa kumwangalia Batuli ambaye alikuwa anatumikishwa kingono na mwajiri wake aitwaye Anti kwa ajili ya kuwastarehesha wateja wake na kumwingizia kipato mama huyu. Batuli anakubaliana na hali hii kutokana na hali ngumu ya kiuchumi inayoikabili familia yake. Vilevile, mwanamke anatumiwa kama chombo cha starehe pale Grace anaposhawishiwa, kuwa na uhusiano ya kimapenzi akiwa bado mwanafunzi na Nashon. Na baada ya kupata ujauzito anatelekezwa na kijana huyu huku akilia na kuonesha uchungu anasema; "Nashon pamoja na starehe zote nilizokuwa nikikupatia leo unanigeuka na kunitupa.'' Maneno haya aliyasema Grace pale baada ya kumweleza Nashon kuwa anaujauzito wake hivyo anaomba washirikiane katika kukabiliana na tatizo hili lakini aliambulia matusi na kufukuzwa.

Taib (2008:133) anasema kwamba fasihi haitoki katika ombwe tupu bali hutoka katika zao la jamii ambalo limejengeka na hali halisi ya maisha ya jamii husika, yaani mtu na mazingira yake ndio Alfa na Omega ya fasihi. Katika jamii ya Kitanzania suala la wasichana kupewa mimba na kukataliwa limekuwa kama jambo la kawaida, kwani wanaume wengi huwatumia wasichana kujistarehesha na pindi wapatapo ujauzito, mapenzi na starehe uishia hapohapo mzigo wote huachiwa mwanamke aubebe mwenyewe bila kujali ataubeba vipi na kwa namna gani. Vivyo hivyo, katika filamu ya *White Maria* dhana ya mwanamke kama chombo cha kustarehesha ulimwengu inajidhihirisha pia ambapo Prof.Dumba alimbaka Anna, kwa ajili ya kujistarehesha yeye mwenyewe.

Hughes (2000:1) anaeleza kwamba kuwatawala wanawake na wasichana katika masuala ya mapenzi kunatengeneza unyanyasaji wa wanawake kijinsia, duniani pote. Anazidi kufafanua kwamba wanaume wamechukua nafasi ya kufanya maamuzi katika nyanja zote katika taasisi za kijamii, kisiasa na kidini ambazo ndizo zinazounda na kuitawala jamii. Kupitia mamlaka ya taasisi hizi, wanaume wameunda utamaduni, sheria, na sera ambazo zinawasaidia katika maslahi yao ya kuwatawala wanawake na watoto katika umma mzima na kwa mtu binafsi. Suala hili linaweza kujadiliwa kwa undani zaidi kwa kuhusishwa na ubidhaishwaji wa karibu kila kitu katika mfumo wa kibepari. Mfumo huu hugeuza kila kitu kuwa bidhaa ya kuuzika sokoni kiasi kwamba wenye nguvu wanauza nguvu zao kwenye mieleka na ngumi, wenye mbio wanauza mbio hizo, wenye sauti pia huziuza sauti zao, wenye urembo huuza urembo wao, wafanyakazi huuza jasho lao, na wale wasio na chochote zaidi ya miili waliyonayo huiuza miili hiyo.

## 4.4 Dhamira Zinazohusu Mwanamke Katika Filamu Teule

Baadhi ya waandishi wa kazi za fasihi wanakubaliana kuwa vipengele vya kifasihi ndivyo huwa vijenzi vya maana ya utungo na hufanya kazi ya kuumba dhamira. Kwa hakika suala la dhamira kama viini vya tungo za kisanaa ndilo linalosawiri ndani ya kazi ya fasihi. Mbonde (1999) anasema kuwa fasihi huweza kuwa na dhamira zaidi ya moja. Hii imejitokeza pia katika semi zilizoandikwa katika daladala ambapo zina dhamira mbalimbali. Baadhi ya watu huchanganya dhamira na maudhui katika kazi ya fasihi. Watu wengi huzungumzia maudhui wakimaanisha dhamira, ingawa ni vitu viwili tofauti. Kwa hakika, dhana ya dhamira hutumiwa kuelezea wazo kuu katika kazi za kifasihi na wazo kuu huusiana na lengo la mwandishi wa kazi hiyo na pia huhusika na dhamira ndogondogo. Katika uchambuzi wa dhamira zihusuzo

mwanamke katika filamu hii teule, utafiti huu umegundua kuwa dhamira hizo zimejitokeza katika pande mbili, upande wa kwanza mwanamke amesawiriwa katika hali hasi, na upande wa pili mwanamke amesawiriwa katika hali chanya.

### 4.4.1 Dhamira Zinazomsawiri Mwanamke katika Hali Chanya

Katika uchambuzi wa filamu teule utafiti umebaini kuwepo kwa dhamira zianazoonesha uchanya katika kuakisi maisha halisi ya wanawake katika jamii. Tunapozungumzia dhamira zenye kuakisi hali chanya kwa mwanamke tunajikita katika dhana ya uchorwaji wa mwanamke kwa kuangalia namna mwanamke anavyochukuliwa na jamii kimajukumu. Aidha kupitia mahojiano na kundi lengwa. Matokeo yanaonesha kuwa katika filamu teule za Steven Kanumba dhamira zinazomsawiri mwaname katika hali chanya zimejidhihirisha katika masuala ya msimamo, mtazamo, maamuzi, uwajibikaji katika mambo ya kijamii namna mira na desturi zinavyomchukulia kwa uzuri na ustawi bora wa kijamii. Katika filamu teule, mwanamke amechorwa katika mitazamo mbalimbali huku akisawiriwa kuwa mtu muhimu katika jamii kama inavyojadiliwa katika vipengele hivi.

#### 4.4.1.1 Uvumilivu na Ujasiri

Kutokata tamaa, ujasiri na uvumilivu kwa mwanamke kunajitokeza kwenye kazi mbalimbali za fasihi. Kwa mfano katika riwaya ya *Watoto wa Mama Ntilie,* (2002) mhusika Mama Ntilie anachorwa kuwa mvumilivu, jasiri na asiyekata tamaa ya maisha. Hii inajidhihirisha kwa jinsi anavyoweza kuvumilia matatizo ya ulevi wa mume wake bila kukata tamaa. Anaamua kufanya biashara ndogondogo kwa lengo la kutokomeza umaskini unaoikabili familia yao. Katika riwaya hii pia Kurwa ni mmoja wa wahusika wavumilivu na jasiri katika kuyakabili matatizo. Katika filamu teule ya *Fake Smile,* dhamira hii inajidhihirisha kwa kumwangalia mhusika mama

Batuli ambaye anaonyesha ujasiri katika kupambana na changamoto ambazo zinamkabili. Mbali na kutelekezwa na wanaume waliomzalisha watoto wawili, mama huyu hakukata tamaa. Aliendea kuwalea watoto wake huku akijishughulisha na upikaji wa vitumbua ili aweze kujipatia kipato cha kutunza familia yake. Halikadhalika Batuli aliendelea kuwa mnyenyekevu na mvumilivu mbali na matatizo na manyanyaso yote aliyoyapata kutoka kwa mdogo wake Betha. Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu inaonesha kwamba wanawake wengi wanakumbana na tatizo hili la kuyabeba matatizo ya kifamilia moyoni na kuyavumilia hata pale ambapo atakuwa anajiumiza mwenyewe. Hivyo, nadharia hii imesaidia kuyaweka wazi matatizo wanayoyapata wanawake ili yaweze kutatuliwa. Ni dhahili kuwa wanawake wengi wamekuwa wakipata matatizo kadha wa kadha katika jamii zao lakini wamekuwa wakipambana bila kukata tamaa wala kurudi nyuma.

#### 4.4.1.2 Misimamo katika Maisha

Katika utafiti wetu tumebaini kwamba katika filamu teule mwanamke amesawiriwa kama kiumbe mwenye msimamo, ambapo msanii amemtazama mwanamke kama mtu mwenye kusimama thabiti katika kile anachokiamini katika uhalisia wa maisha yake. Mathalani Bi Catherine (mke wa Conrad) ameonesha msimamo pale mumewe alipokuwa akimshawishi atafute mtu wa kumsaidia kazi za ndani aligoma na kudai kazi zote anaziweza hivyo haina haja ya kuwa na mfanyakazi. Vile vile, aligoma kwenda kwa mganga wa kienyeji kutafuta dawa ya matatizo yaliyokuwa yakiikumba familia yake na kumtaka mumewe waende kanisani wakaombewe. Kwahiyo mtunzi wa filamu hii teule anatambua nafasi ya mwanamke katika jamii hasa katika kusimamia kile aaminicho kuwa ni cha kweli katika jamii. Athari anayoipata hapa

mwanajamii ni chanya ambayo ni kuwa na msimamo katika maisha. Hivyo kudhihirisha kuwa Nadharia ya Ufeministi wa Dunia ya Tatu imeanza kufikia malengo, mwanamke hawezi kuyumbishwa kimsimamo kwa namna rahisi hivyo kwani ni mtu imara

#### 4 .4.1.3 Staha na Usiri

Siri ni moja ya mambo muhimu katika mahusiano ya watu, katika jamii. Hali hii inaonesha kwamba dhana ya kuficha ama kutuza siri ni muhimu sana katika maisha ya mwanadamu na kwamba yapo mambo ambayo yanapaswa kuelezwa kwa watu wengine lakini yapo mambo ambayo kwa sababu ya unyeti wake na usalama wake halipaswi kutolewa ama kusimuliwa kwa mtu mwingine. Mathalani kuna siri za ndani sana za maisha ya ndoa, kuna mambo ya siri ya kifamilia, mathalani kuna mambo ya siri ya kiofisi na hata serikalini. Aghalabu siri huwa ni kwa ajili ya kiusalama na heshima. Hali hii hutokana na ukweli kwamba iwapo jambo hilo litasemwa na kuwafikia watu wengine, huweza kulitumia kubomoa na kuhatarisha usalama na amani iliyopo katika jamii au familia husika. Mtunzi wa filamu hii ya *White Maria* amempa mwanamke heshima kubwa kwa kumchora kama kiumbe mwenye kutunza siri.

Katika filamu hii teule, mke wa Conrad ameonesha kuwa ni mtunza siri kwani aliweza kuyaficha matatizo yaliyokuwa yakitokea katika familia yake, ambapo mumewe alikuwa akitokewa na mzimu wa Maria ukimtaka kukili makosa yake yote aliyomtendea Maria na wasichana wengine wakati wa uhai wao. Umuhimu wa kutunza siri unaonekana kwa sababu iwapo mwanamke ataanza kutoa siri nje ya mambo yanayotokea katika familia yake basi itakuwa rahisi maadui kuvunja ndoa yao. Hii ni kwa sababu kati ya watakaoipata siri hii wapo watakaotoa ushauri

kwamba achana na huyo mwanaume njoo kwangu, wengine watakwambia achana nae rudi kwenu pamoja na kuwa yapo mambo mengi yanayopelekea ndoa kuwa hatarini kuvunjika. Pamoja na hayo ni vyema kwa mwanamke kuwa makini na siri anayoifumbata. Sio kila jambo linafaa kuwa siri kwani wakati mwingine linaweza kusababisha kukosekana kwa haki za msingi au kuleta madhara. Kwa mfano Muhando, (1974) katika tamthiliya ya *Heshima Yangu* amemchora mama Salum kuwa ni mama anayetunza siri ya ujauzito wake kwa muda mrefu bila kumtaja hadharani mtu aliyempa mimba hiyo. Mama Salum alikaa na siri hiyo tokea aliposhika ujauzito, alipojifungua na kulea mtoto wake hadi kufikia umri wa kuoa. Aliamua kuitunza siri hii kutokana na kuhofia vitisho alivyofanyiwa na mzee Issa, ambaye ndiyo mhusika wa ujauzito huo. Suala ambalo lilisababisha mtoto huyo kupendana na dada yake jambo ambalo ni kinyume na maadili ya jamii kuoana ndugu wa baba mmoja. Utafiti umebaini kuwa dhamira ya msanii ni kuwa kutunza siri ni muhimu katika nyumba kwa ajili ya usalama na mwanamke amefanikiwa kuwa mtunza siri katika jamii.

#### 4.4.1.4 Uadilifu na Uchamungu

Suala la uadilifu na uchamungu limeonekana kuwa njia inayoweza kumkomboa mwanadamu dhidi ya tamaa, ufisadi, ubinafsi na matatizo mengi ya maisha yanayoikumba jamii. Uadilifu na uchamungu umeonekana kuwa suluhisho la maisha na unatoa mwangaza juu ya tabia zinazofaa kufuatwa kama kuaminiana, kuheshimiana, kupendana na kuwa na nia safi. Katika filamu ya *White Maria*, bi Catherine amesawiria kama mcha mungu na anayeamini katika dini ya Kikristo. Hii inajidhihirisha kwa kumwangalia mke wa Conrad ambaye anaonekana akisoma Biblia na kufanya maombi kwa kutegemea sana nguvu za Mungu kutokana na

mikosi na matatizo yanayoiandama familia yake. Bi Catherine anapopata matatizo na kukosa amani katika familia, anaamua kumuita mchungaji na kufanya maombi huku akimuombea mumewe ambaye ni mgumu kwenda kanisani abadilike na kuwa mcha mungu ndipo matatizo yanayowaandama yatakapokoma na kuisha. Catherine anaamini kwamba ukiwa na imani kwa Mungu yote yanawezekana kupitia imani yake na nguvu ya maombi, hatimaye mumewe aliamua kwenda kanisani kutubu dhambi zake na matatizo yote yaliyowaandama yalikwisha. Utafiti umebaini kuwa mtunzi amemchora mwanamke kuwa kiumbe mshika dini na ni mwenye kumwamini sana mungu katika kutatua matatizo.

#### 4.4.1.5 Malezi

Jukumu la uzazi na ulezi ni la mwanamke mwenyewe katika utamaduni wa jamii nyingi (Sen, 1995). Sen anazidi kueleza kwamba katika tabia ya kifamilia usawa kati ya wanaume na wanawake haupo na kukosekana kwa usawa huo kunaonekana kama jambo la asili lisiloweza kubadilika. Utafiti huu umebaini kuwa mwanamke ni mlezi wa familia. Mtunzi ameonesha nafasi ya mwanamke kuwa ndiye mwenye nafasi kubwa katika malezi ya watoto na familia kwa ujumla. Mathalani katika filamu teule ya *Fake Smile* mwanamke amesawiriwa kama mlezi wa familia kwa kumtumia mhusika mama Batuli ambaye aliweza kuwalea watoto wake peke yake bila kupata msaada wowote toka kwa baba zao. Pamoja na kukumbana na changamoto mbalimbali lakini hakukata tamaa. Hata hivyo, wanaume wengine ni wakali na wakorofi hata kama wake zao wamewaomba kwa upole wawasaidie baadhi ya kazi nzito wanaweza hata kuwapiga wakidai kwamba wanawake hao hawana adabu tena ni jeuri. Lakini hata hivyo yote hayo yanasababishwa na mfumo dume uliopo katika jamii.

Felluger (1998) anaelezea kuwa, mfumo dume ni utawala wa kibaba, na mtazamo mkuu wa ustaarabu wetu unaoonea, unaotawaliwa, unaoundwa na kuongozwa na wanaume. Hii ni kwa sababu ya kuwafanya wanawake kuwa wasaidizi wa wanaume katika nyanja zote za maisha. Kwa mfano, wapo wanawake wengi wanaishi maisha kama ya mama Batuli kwa kuuza vyakula, wengine wanafanya shughuli za kilimo na biashara nyingine ndogondogo ili waweze kujikwamua katika matatizo ya kiuchumi. Fedha wanazozipata wanazitumia katika kulipia ada za watoto wao na kuongeza pato la familia. Tabia za akina baba wengi kutelekeza familia zao kwa sababu mbalimbali, huwasababishia akina mama, kuwa na mzigo mkubwa wa kulea familia. Jamii ya Kitanzania hususani wanawake, wanapaswa kuwa makini katika kutafuta mbinu faafu za kujikwamua kiuchumi na katika matatizo mengine pia.

#### 4.4.1.6 Huruma na Utu

Dhana ya huruma kwa mwanamke imejitokeza sana katika kazi za fasihi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba picha hii inasawiri maisha halisi ya mwanamke kuwa kiumbe mwenye huruma. Mwanamke amesawiriwa kama mtu mwenye huruma hata kama huruma anayokuwanayo inamuumiza yeye mwenyewe. Mathalani Batuli alionesha huruma kwa mama yake pale mama yake alipokuwa mgonjwa hana hela yakununua dawa wala ya kulipa kodi ya nyumba. Batuli aliamua kwenda kufanya kazi za ndani ambapo katika kutafta namna ya kumuokoa na kumsaidia mama yake ndipo alipokumbana na udhalilishaji wa kijinsia kwa kufanyishwa biashara ya ukahaba na tajiri yake. Hakuwa na namna ya kukataa aliamua kukubali ili amsaidie mama yake katika kupata matibabu. Kutokana na huruma yake Batuli alihatarisha maisha yake ili aweze kumuokoa mama yake. Aidha, dhana ya huruma kwa mwanamke imebainishwa na hata na waandishi wa kazi mbalimbali za fasihi huku

wakimchora mwanamke kipekee sana. Mathalani riwaya ya *Takadini* ya Ben J.henson imemchora Sekai kuwa mwanamke mwenye huruma hasa anapoamua kumtorosha mwanae Takadini ambaye alikuwa Sope na hasiyetakiwa kuishi kutokana na mira na desturi za jamii yao. Mwandishi ameonesha jinsi mwanamke alivyoamua kuhatarisha maisha yake kwa kutembea usiku na mchana porini ili kuyaokoa maisha ya mtoto wake Takadini. Hivyo basi suala la huruma kwa mwanamke ni la kiuhalisia katika jamii za Kitanzania

### 4.4 .2 Dhamira Zinazomsawiri Mwanamke Katika Hali Hasi

Usawiri wa mwanamke katika kazi nyingi za sanaa haukuonyesha tu uchanya wa mwanamke bali pia ulionyesha uhasi huku hali yake ikidunishwa zaidi na pengine hata kuhusishwa na vyanzo vya migogoro katika jamii, Jilala (2011) ameonyesha jinsi mwanamke anavyoweza kuchorwa kitaswira zinazolenga lawama dhidi ya mwanamke. Mathalani ametumia taswira ya Dege la Jeshi mbayo inamlaumu mwanamke kama malaya na chanzo cha maambukizi ya UKIMWI, hivyo anapaswa kuogopwa au kujihami kwa kutumia kondom. Vivyo hivyo, utafiti huu umebaini kuwepo kwa usawiri hasi wa mwanamke na athari hasi katika filamu teule ya. Aidha, uchorwaji wa mwanamke katika athari hasi umejiegeza katika kumuangalia mwanamke katika jicho la kidhaifu katika matendo pamoja na maamuzi.

#### 4.4.2.1 Unafiki na Usaliti

Dhana ya unafiki imejitokeza kwa maana ya kujifanya kwa mtu kuwa na msaada au unasaba na mtu fulani katika jambo fulani lakini kiuhalisia yuko kinyume kabisa. Utafiti huu umebaini kwamba mwanamke amechorwa kama kiumbe mnafiki mwenye tabasamu la bandia, huku akijivika ngozi ya kondoo kumbe ndani ni mbwa mwitu. Mathalani mhusika Batuli katika filamu ya *Fake Smile* anaonekana kuwa ni

mwanamke mnafiki kwa kujifanya anampenda Bosco kumbe sivyo. Moyo wake ulimpenda Benjamini hali iliyosababisha kuwa anachukua pesa kwa Bosco na kumpa Benjamini. Mhusika huyu alikuwa mpole, mnyenyekevu na mwenye tabasamu zuri, lakini hayo yote yalificha uovu aliokuwa nao.

Usawiri wa mwanamke kuwa mnafiki ni moja ya dhana zinazokumba jamii za leo hasa katika kipindi hiki cha teknolojia ya digitali ambapo maadili yamemomonyoka na sehemu kubwa jamii imekengeuka.Vivyohivyo, kwa upande mwingine mwanamke ameonekana msaliti na mwepesi wa kushawishika. Mtunzi ameweka wazi suala la usaliti kwa mwanamke kwa kutumia mhusika Batuli ambaye alibadilika kitabia baada ya kufika chuoni na kukutana na Benjamini alisahau yote aliyotendewa na Bosco na kuanza kutembea na Benjamini hali iliyopelekea kupata maambukizi ya VVU (Virusi Vya UKIMWI). Madhara ya usaliti na udanganyifu katika ndoa au uhusiano kwa ujumla yanaweza kufarakanisha familia kwa kuleta migogoro isiyokwisha na kurudisha maendeleo nyuma kutokana na kukosa umoja kati ya watu. Kwa jumla, usaliti, utapeli na udanganyifu katika uhusiano wa kimapenzi hutokea kwa kiwango kikubwa katika jamii ya Kitanzania. Wapo wasichana wadogo na wanawake ambao wanasaliti wapenzi wao na hata ndoa zao kutokana na kutawaliwa na tamaa ya mali, matokeo yake huishia kutendwa vibaya huku wakijuta. Ndipo utimiapo usemi usemao kwamba tamaa mbele mauti nyuma. Vivyo hivyo, suala la unafiki na usaliti limejidhihirisha katika filamu ya *White Maria* Utafiti wetu umebaini kwamba mwanamke amechorwa kama kiumbe mnafiki kwa kujifanya anashirikiana na mhusika huku moyoni akiwa kinyume, bali alikuwa na mpango wake mwingine. Mathalani mke wa Onesmo anaonesha unafiki pale anapokubaliana na mumewe kuwa amekubali kuishi pamoja na Joyce kama mke mwenzake. Na atatoa ushirikiano wote katika kulea ujauzito alionao Joyce, kumbe moyoni aliwaza

kinyume ndipo baadaye anapoamua kumuua Joyce pamoja na mwanaye aliyeko tumboni. Kutokana na hali hii msanii anaonesha kuwa wanawake badala ya kutendeana mema na kusaidaina wanakuwa wanadhuliana wao kwa wao kisa wivu wa mapenzi na ubinafsi. Usawiri wa mwanamke kuwa mnafiki ni moja ya dhana zinazokumba jamii ya leo ambapo maadili yamemomonyoka na ubinafsi umechukua nafasi kubwa

**4.4.2.2 Utovu wa Maadili**

Suala la maadili ni jambo ambalo linajenga utu wa mwanadamu, kwani umaanisha kuwa mtu mwenye maadili ndiye mwenye utu. Suala la malezi bora, adabu, heshima, hekima na utu ni vitu ambavyo vinaendana na vina uhusiano wa karibu. Katika filamu teule mwanamke amesawiriwa kama mtovu wa maadili asiye na malezi bora na utu.

Katika filamu ya *Fake Smile* matendo ya mhusika Betha yanadhihirisha utovu wa maadili kwa mwanamke. Kwani anaonekana ni mtu asiye na adabu, heshima, hekima utu na maadili kwa dadayake, mama yake pamoja na watu wengine. Hii inajidhihirisha pale ambapo Betha anashindwa kumsaidia dadayake kazi nyumbani huku akidai kuwa katengeneza kucha zake hataki zichafuke, na kudai kuwa hatahivyo dadayake ni *housegirl* mzoefu hivyo kazi zote atazimudu. Vilevile, anaonesha utovu wa nidhamu kwa kudharau chakula alichonunua mama yake na kudai amechoka kula vyakula vya aina moja kila siku wakati hali halisi ya maisha ya mama yake anaitambua..

Katika jamii ya Kitanzania suala la utovu wa maadili kwa wanawake lipo. Hii ni kutokana na malezi wapewayoa na wazazi wao kwani baadhi ya wazazi wanawalea watoto wao katika maadili yasiyomema na kuwasababishia kukosa upendo, moyo wa

kujali wengine na hatimaye kukosa heshima na hekima, kwani mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Hali hii inatokana na kukosekana kwa ushirikiano katika malezi ya watoto baina ya wazazi wote wawili yaani baba mama. Mfano unakuta baba anamwachia mama pekee jukumu la malezi ya watoto na ikitokea wakaaribikiwa kimaisha mama ndiye mwenye kubeba mzigo wa lawama. Nadharia ya Ufeminsti wa Nchi za Dunia ya Tatu inapinga kazi zinazoendeleza mfumo dume. Kama inavyooneshwa hapo juu kuwa jukumu la malezi ya watoto ni la mwanamke peke yake. Hivyo basi, nadharia hii inasisitiza usawa katika mgawanyo wa majukumu likiwemo suala la malezi ya watoto.

#### 4.4.2.3 Ushirikina na Uganga

Katika uchambuzi wa filamu ya *White Maria* mwanamke amesawiriwa kuwa na imani za kijadi yaani ushirikina. Hii inajidhihirisha kwa kumwangalia Sekretari wake Conrad anapomshawishi Conrad waende kwa mganga wa kienyeji ndiye atakayetatua matatizo yake. Anamuua kumpeleka kwa mganga wa kienyeji ambaye anawapatia dawa hata hivyo hazikutatua matatizo ya Conrad. Katika jamii wapo wanawake ambao wanategemea nguvu za uchawi na uganga katika kutatua matatizo yao mbalimbali. Wanawake wengi hasa waishio vijijini na maskini wanaamini sana ushirikina. Pia mijini baadhi ya wanawake wanaamini kuwa nguvu za usihiri zinaweza kuwasaidia kuwafanya wanaume wawe chini yao na kila watakachoongea ama kuda, mwanaume akubaliane naye. Usawiri wa mwanamke kuwa mtu anayeamini ushirikia na uganga ni moja ya dhana zinazoikumba jamii wakati huu, ambapo wanawake wengi wanendekeza sana uganga na ushirikina.

#### 4.4.2.4 Ukatili na Mauaji

Kama inavyooneshwa katika chambuzi mbalimbali za kifasihi za Kiswahili ambapo mwanamke huvikwa husika na matendo mbalimbali yenye kumuonesha kama mtu katili, muuaji, laghai, msaliti pamoja na mambo mengine yenye kumfanya aonekane duni na dhalili. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, hali ya kundunisha mwanamke inatokana na utamaduni wa Kiafrika ambao kwa kawaida humweka mwanamke katika daraja la chini dhidi ya mwanaume. Suala la ukatili wa mwanamke katika filamu ya *White Maria* limeonekana pale mke wa Onesmo alimpomuua mfanyakazi wake wa nyumbani, Joyce, wakati alipokuwa anaumwa uchungu wakati wa kujifungu. Alimziba kwa kutumia mto, mpaka akapoteza uhai kisa wivu wa mapenzi kwani Joyce ujauzito aliokuwa nao ni wa mumewe bwana Onesmo. Katika jamii ya Kitanzania wanawake wanachukuliwa katika nafasi mbalimbali. Wapo wanawake wanaotaka kujikomboa kutokana na matatizo mbalimbali kwa kujikwamua wao wenyewe. Hawa wanawakilisha ukombozi wa mwanamke ingawa wanakabiliwa na changamoto ili kufikia malengo yao. Wanawake katika kundi la pili wanataka kupata huduma muhimu kwa kuuza miili yao lakini mwisho wake wanaishia kupata ujauzito na maradhi. Pia kundi lingine la wanawake ni lile la wenye roho za kinyama, ambalo linadhamiria kudhuru na kuumiza wanawake wengine. Kwa hakika, wanawake wanapaswa kuenenda katika njia inayofaa, inayopaswa na kuweza kuigwa na watu wengine katika jamii. Hivyo basi, wasijidhalilishe kwa kujiona kuwa wao ni viumbe duni bali wajitahidi kujikomboa kwa kujikwamua kwa kufanya shughuli za kiuchumi na kuepuka utegemezi Katika jamii ya Kitanzania, suala la wanaawake kuwa wakatili lipo sana kwani ni mara kadhaa vyombo vya habari vinaripoti, katika sehemu kadhaa wanawake kuwaua na kuwatesa watoto wao wa kambo, hii inatokana na hali ya ubinafsi na wivu walionao wanawake. Ili kutimiza malengo ya

wananadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu ambayo ni ukombozi wa mwanamke, wanawake hawana budi kupendana na kuthaminiana.

#### 4.4.2.5 Umaskini

Umaskini ni ukosefu wa mali, ufukara na ukata (TUKI 2004). Umaskini ni miongoni mwa matatizo makubwa yanayozikumba nchi zinazoendelea. Kutokana na kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo, umasikini unajitokeza kwa kiasi kikubwa na kuathiri maisha ya watu. Watanzania walio wengi ni masikini sana mpaka kiasi cha kushindwa kumudu maisha yao na kuacha urithi wowote wa mali kwa watoto wao (Chiraka, 2009:54). Umaskini umesababisha watu wengi kushindwa kupata elimu. Zipo kazi mbalimbali za sanaa ambazo zimezungumzia suala la umaskini. Katika filamu ya *White Maria* suala la umaskini kwa mwanamke limejitokeza kwa kuangalia maisha ya Anna na Joyce. Umaskini wa familia ya akina Anna ndio uliosababisha binti huyu kushindwa kupata elimu na badala yake aliendа kufanya kazi za nyumbani kwa Prof. Dumba, ambapo nako aliambulia kubakwa na kupewa ujauzito na kufukuzwa. Naye Joyce baada ya mama yake kufariki anakuwa mtoto asiye na makazi maaluumu na ombaomba. Umaskini unaweza kusababisha watu kujiingiza katika mambo ambayo yanahatarisha maisha yao. Kwa mfano, wapo wasichana waliojiingiza katika masuala ya mapenzi ili waweze kupata fedha za kujikimu. Hali hiyo huwaweka katika mazingira hatayarishi ya kuweza kupata ugonjwa wa UKIMWI na madhara mengine mengi.Nadharia ya Ufeministi wa Nchi za Dunia ya Tatu inapigania haki na usawa wa kijinsia katika Nyanja mbalimbali likiwemo suala la kupata elimu na ajira. Hivyo, basi endapo mwanamke atapata elimu ataweza kuepukana na tatizo la umaskini kwani ataweza kujiajiri ama kuajiriwa.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kujadili matokeo ya utafiti. Aidha, imewasilisha na kujadili namna mbalimbali za usawiri wa mwanamke katika filamu teule, mtazamo wa jamii juu ya mwanamke kupitia filamu teule. Vilevile, imejadili dhamira mbalimbali zinazohusu mwanamke katika filamu teule. Katika uchambuzi data, zimeshadidiwa na Nadharia ya Ufeministi ambayo imekuwa mhimili mkubwa katika kuchakata data za utafiti huu. Sura ifuatayo itaeleza muhtasari wa kazi nzima, ikiwa ni pamoja na maoni na mapendekezo ya mtafiti kwa wanawake, jamii, pamoja na mapendekezo kwa watafiti wengine.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari, mapendekezo na hitimisho la matokeo ya utafiti. Sura inaundwa na sehemu kuu nne ambazo; muhtasari wa matokeo ya utafiti, utoshelevu wa nadharia iliyotumika, mapendekezo kutokana na utafiti na hitimisho.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo kwa kujikita zaidi katika filamu teule mbili za Steven Kanumba. Na kubainisha ni kwa namna gani mwanamke amesawiriwa katika filamu hizo na uhalisi wake katika maisha ya jamii ya kila siku. Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla, ufafanuzi wa istilahi zilizotumika, usuli wa tatizo ambao unaeleza historia ya filamu nchini Tanzania pamoja usawiri wa mwanamke katika kazi za kifasihi kwa ujumla. Tatizo la utafiti limeelezewa sanjari na malengo ya utafiti ambayo yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni lengo kuu na malengo mahususi ambayo yako matatu. Malengo hayo matatu yamezalisha maswali ya utafiti ambayo nayo yako matatu. Maswali hayo yamejibiwa katika uchanganuzi wa data na hivyo malengo ya utafiti yakatimizwa. Nadharia ya utafiti pia imeelezwa. Umuhimu wa utafiti umeoneshwa na kuelezea jinsi wataalamu mbalimbali, wanafasihi, wasomaji na watafiti watakavyofaidika. Vilevile, maelezo mafupi kuhusu Steven Kanumba yameelezwa. Mwishoni, kuna mpangilio mzima wa utafiti.

Sura ya Pili ya tasnifu hii inahusu mapitio ya maandiko. Maandiko kuhusu usawiri wa mwanamke, maandiko kuhusu filamu kwa ujumla yameelezwa. Mwisho, imeeleza kuhusu mapengo yaliyojitokeza. Sura ya Tatu ya tasnifu hii inaelezea

mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika kukamilisha tasnifu hii. Mbinu hizo ni pamoja na usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli, vifaa vya utafiti sambamba na njia za ukusanyaji wa data.Itikadi na udhibiti wa data pamoja na vikwazo vya utafiti vimeelezwa pia katika sura hii.

Katika Sura ya Nne ya tasnifu ndipo data zilipojadiliwa. Uchanganuzi wa data hizi ndio uliojibu maswali ya utafiti sambamba na kutimiza malengo ya utafiti yaliyokusudiwa. Data zote zilizopatikana maktabani zilichambuliwa na kuweka bayana usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo. Usawiri wa mwanamke umeelezewa kwa uwazi kwa kushadidiwa na Nadharia ya Ufeministi. Mwisho tasnifu hii imejengwa na sura ya tano ambayo inatoa muhtasari wa tasnifu nzima, inahitimisha na kutoa mapendekezo kwa watafiti, wataalamu, wasomaji na jamii kwa ujumla. Katika utafiti huu, imegundulika kwamba nafasi ya mwanamke katika tasnia hii ya filamu, anakandamizwa na kudharauliwa na kufanyiwa vitendo vya kidhalili. Aidha, utafiti huu umegundua kuwa vitendo vya kidhalili na unyanyasaji atendevyo mwanamke havitendwi na mwanaume pekee bali pia mwanamke anahusika katika kumnyanyasa mwanamke mwenzake.

Katika asasi zote mwanamke ameonekana kukandamizwa na kudunishwa katika kupata elimu, ajira, pamoja na suala zima la uzazi na malezi hii yote inatokana na mfumo dume uliopo katika jamii.Yote haya yamesababishwa na mwanamke kukosa urazini kuhusu haki zake. Hali hiyo ndiyo iliyowaamsha wanawake mafeministi kuanza harakati za kujikomboa ili waweze kutokana na hali ya kugandamizwa. Katika upande wa mgawanyo wa majukumu, mwanamke ameonekana kuwa hawezi kufanya kazi ambayo ni ya mshahara sawa na mwanamume. Pia mwanamke anaonekana kuachiwa kazi zote za nyumbani ambazo hazina ujira wowote. Kazi hizo hazithaminiwi kuanzia ngazi ya familia mpaka ngazi ya jamii, kama zilivyo za

wanaume. Hata ikiwa mwanamke amepata kazi lakini mshahara wake hauwezi kulingana na wa mwanaume, mwanamke analipwa mshahara mdogo zaidi kwa kuwa anaonekana kuwa hawezi. Hata hivyo, mwanamke hajasawiriwa katika hali hasi pekee bali pia amesawiriwa katika hali chanya kama vile mlezi wa familia, mshauri, mtunza siri na mvumilivu.

Utafiti huu umetoa mwanga kwa wanawake waandishi wa fasihi na wale wasio wanafasihi ila wanaandika kuhusiana na wanawake, kwani tasnifu imeweza kugusa pande zote za kifasihi na zile zisizo za kifasihi. Pia utafiti huu umeonnesha waziwazi dhamira zenye kumsawiri mwanamke katika nafasi hasi na zile zenye kumsawiri mwanamke katika nafasi chanya zilivyojitokeza katika filamu teule.

## 5.3 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Utafiti huu umetumia nadharia ya Ufeministi ili kuweza kuibua masuala ya usawiri wa mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba. Mawazo ya nadharia hii kuhusu mfumo dume na nafasi ya mwanamke mfano, mawazo ya nadharia hii yanaeleza kwamba, mwanamke amekuwa mhanga wa mfumo dume ambao unamtazama mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume na kumkosesha fursa mbalimbali kama vile elimu, ajira na kumiliki mali. Kutokana na mawazo haya tumeweza kuona katika filamu teule wanaume walivyopewa daraja la juu ukilinganisha na wanawake. Hata hivyo wananadharia hii ya Ufeministi wamekuwa wakifanya harakati mbalimbali kumkomboa mwanamke. Matunda ya juhudi zao tumeyaona namna yalivyochangia katika kubadili hadhi ya mwanamke katika jamii kwa sasa mwanamke halisi wa Kitanzia anashiriki katika siasa, uongozi, ujasiliamali, pamoja na kupata ajira tofauti na zamani.

Hii yote ni mafanikio ya mafeministi katika kumkomboa mwanamke. Ni dhahili kuwa nadharia hii imejitosheleza vizuri katika uchambuzi wa data kwa sababu malengo mahususi matatu ya utafiti huu yameweza kukamilika kama ilivyokusudiwa. Tunayasema haya kwa sababu tumethibitisha, kwamba mwanamke wa sasa anashiriki katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na kujiletea maendeleo endelevu anashiriki katika siasa uongozi na uongozi wa ndani na nje ya nchi mambo haya zamani yalifanywa na wanaume peke yao wakati wanaume wakitekeleza majukumu haya wanawake walifanya kazi za kupika chakula, kuosha vyombo, kusafisha nyumba, pamoja na kuzaa na kulea watoto pamoja na kazi nyinginezo ambazo hazimwingizii kipato mwanamke. Kwa msingi huu mawazo ya mafeministi yenye msimamo mkali dhidi ya kumkomboa mwanamke yametuwezesha kukamilisha kazi yetu ya utafiti wetu.

## 5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti

Kutokana na utafiti uliofanyika mambo yafuatayo yanatolewa mapendekezo:

### 5.4.1 Mapendekezo kwa BASATA

Kwa kuwa tasnia ya sanaa iko chini ya usimamizi wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) inapendekezwa kwamba, Baraza la Sanaa litoe maelekezo kwa wasanii hasa juu ya mambo muhimu yanayofaa kuwasilishwa kwa jamii na mavazi yanayofaa kuvaliwa katika utambaji wa wa kazi zao. Pia inashauriwa kuwa BASATA wawe na utaratibu wa kutoa semina elekezi kwa wasanii na watunzi wa filamu kuhusiana na namna ya kumsawiri mwanamke katika kazi zao na kuelimisha kuhusu suala zima la ujinsia. Hali hii itatunza heshima ya utamaduni wa Kitanzania na Uafrika kwa ujumla pamoja na utu wa mwanamke.

### 5.3.2 Mapendekezo Kwa Mtandao wa Jinsia Tanzania

Wanawake ni watu walio duni mbele ya wanaume kwani jamii ndivyo inavyowaona. Uduni wao ndio unaowafanya wasipate kazi za kuajiriwa kwa wingi kama walivyo wanaume. Ingawa jamii imeanza kufunguka na kuona umuhimu wa mwanamke katika ngazi zote lakini hata katika ajira walio wengi hawapati haki, malipo na nafasi sawa na wanaume. Hii ni kwa sababu wanaume hawaamini kama wanawake wanaweza kama wanaume wanavyoweza. Kutokana na tatizo hili, Mtandao wa Jinsia nchini Tanzania unapaswa utambue kwamba hata wanawake wanaweza hata kama wasipowezeshwa. Mtandao unapewa changamoto ya kuhimiza mabadiliko ili mwanamke naye apate fursa sawa na mwanaume.

### 5.3.3 Mapendekezo kwa Wanawake

Katika filamu zilizotafitiwa imegundulika kwamba wanawake kwa sehemu kubwa wanadharauliwa na kudunishwa. Udhalili huo unafanywa na wanawake wenyewe pamoja na wanaume hii ni kutokana na jinsi jamii inavyowatazama na inavyowachukulia. Pengine dharau juu ya mwanamke inasababishwa na muonekano wa matendo yake ndani ya jamii kuwa si mazuri. Hivyo inapaswa waelewe kwamba fasihi au sanaa nyingine ni kioo cha jamii kinachoonesha mwenendo mzima wa watu ndani ya jamii. Aidha, wanatakiwa kubadilika na kuwa na mwenendo mzuri ili maadili mema yaweze kuonekana kwao na wawe mfano wa kuigwa. Vilevile, wanawake wanatakiwa kupendana na kuthamiana wao ndipo watakapothaminiwa na jamii kwa ujumla. Hata hivyo, jamii inatakiwa ipambane na suala la uchangudoa kwa kuwapatia wanawake kazi zenye malipo mazuri kwani inaonekana kuwa machangudoa wengi wanafanya biashara hiyo kwa sababu hawana kazi zinazoweza kuendesha maisha yao.

### 5.3.4 Mapendekezo kwa Watafiti

Kwa kuwa tasnifu hii ilijikita katika kuangalia usawiri wa mwanamke katika filamu za Kibongo, itakuwa vema kwa watafiti wengine kufanya tafiti zao kuhusiana na tasnia hii katika masuala mbalimbali mfano katika vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza kwenye filamu hizo na kuandika makala, majarida, na vitabu vingi kabisa ili marejeo yawe mengi.

## 5.6 Hitimisho

Utafiti huu umeonesha kuwa filamu za Kibongo ni nyenzo muhimu inayotumiwa na wasanii katika kuwasilisha mawazo yao. Kazi ya filamu za Kibongo ni sawa na ile ya tanzu nyingine za fasihi. Kama ilivyo kwa tanzu nyingine. Filamu za Kibongo zinaburudisha, zinaelimisha, na kuonya juuu ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa wanawake wanaweza ikiwa watawezeshwa na ikiwa watapewa nafasi ya kuweza. Kama jamii itaona umuhimu wa kuwapa madaraka na mamlaka ya kuongoza na kusimamia kazi katika sehemu nyeti pia. Maendeleo yanaweza kutokea katika nchi ikiwa wanawake watapewa nafasi sawa na wanaume katika sekta zote za uongozi yaani kuanzia nafasi ya urais, uwaziri, ubunge, jeshi, na uongozi wa sehemu nyingine mbalimbali

## MAREJELEO


Balisidya, M.L. (1982), "The Image of Woman in Tanzania Oral Literature: A Survey"

katika. Mulokozi (mh), *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Juzuu 49/2 Uk.08.

Birke, L. (1986), *Women, Feminism and Biology: The Feminist Challenge*, Brighton and Wheatsheal.

Chinyere, S.O (1992), "Portrayal of Women in Nigerian Home Video Films: Empowerment or Subjugation?" *Africa Media Review* vol. 6 no. 1

Diawara, M. (1992), *African Politics and Culture.* Bloomington, Indian University Press.

Eagleton, M. (1991), *Feminist Literary Criticism*, London, Longman.

FEMA Magazine, (2010 Des). *Unyanyasaji wa Kijinsia ni nini*? Femina Hip Editorial Office.

Finnegan, R. (1970), *Oral literature in Africa Nairobi*, Oxford University Press, London.

George, G. (2014), "Usawiri wa Mwanamke katika Tamthiliya Teule za Penina Muhando". Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapwa) .

Gumbo, M. (2010), " Use of Costumes in Tanzanian Fiction Films: The Case of Oprah and From China with Love". M.A Dissertation, University of Dar esSalaam (Unpublished)

Hughes, D.M. (2000), *Men Create the Demand; Women Are the Supply*. Lecture on Sexual Exploitation Queen Sofia Center, Valencia, Spain November 2000 University of Rhode Island.

Hussein, E. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim.* Nairobi, Oxford University.

Jarvie, I. (1978), *Movies as Social Criticism Aspect of their Social Psychology,* Scarecrow Press.

Kanganga, M. P. (2007), "A New Trend in Tanzanian Film Making Challenges and Prospects".MA, Theatre Arts, Dissertation, University of Dar es Salaam. (Unpublished.

Kasiga, G (2008), "Tanzania Growing Film Industry and Job Opportunities for Youth", Conference Paper. University of Regina, Canada.

Kawin, B. (1992), *How Movies Work,* Berkley, University of Califonia Press.

Kayoka, C.M (200), ''The Woman in Kiswahili Literature A Feminist Approach," Dar es Salaam, Open University of Tanzania.

Kezilahabi, E. (2003), "Mandhari na Wahusika," katika *Makala za Semina ya Kimataifa* ya *Waandishi wa Kiswahili 111 Fasihi*, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Khatib, M.S. (1982), *Women in Swahili Poetry*, Unpublished articles, SOAS, London.

Khatib, M.S. (1985), *Utenzi wa Mwanankupona, MULIKA* TUKI, UDSM

Khatibu, M.S. (2010), "Chanjo za Matakwa ya Mwanaume katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Usahairi wa Muyaka na Shaban Robert". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapwa).

Kiango, S.D (1982), "Tamthilia za Kiswahili; Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa" katika Mulokozi (Mh) *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Juzuu 49/2. Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

Kimati, F.R. (2014), "Taswira ya Mwanamke katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi kipya Tanzania: Mifano kutoka Nyimbo Teule za Wanamuziki wa Kike".Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapwa).

Kothari, C.R (2008), *Research Methodology*: Methods and Techniques (2$^{nd}$ Revised) New Age International Publishers Ltd, New Delhi.

Lyatuu, J. (2011), " Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya : Ulinganisho wa Riwaya za waandishi wa Kike na Waandishi wa Kiume": Barisidya na Mwanga, Kezilahabi na Mohamed .Shahada ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar-Es-Salaam. (Haijachapwa).

Mackinnon, C.A (1991), *Toward A Feminist Theory of the State*. London, Havard University Press.

Mbogo, E. (2002), *Watoto wa Mama Ntilie.* Dar es Salaam, Heko Publishers Ltd. Mbogo, E. (2002), *Watoto wa Mama Ntilie*. Heko Publishers.

Mbughuni, M. (1982), *The Image Women in Kiswahili Prose and Fiction BRALUP* Paper No. 26, UDSM.

Mhando, M (2010): "Creative/Cultural Industries Financing in Africa: A Tanzanian Film Value Chain Study." *Journal of African Cinemas* Vol 2 No 1. Doi:

Mlama, P. (1976), *Hatia*, Dar es Salaam, East African Publishing House.

Mlama, P. (1982), *Nguzo Mama*, Nairobi OUP.

Momanyi, C. (1998) "Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili".Phd. ThesisNairobi. Kenyatta University (Unpublished).

Mponguliana, J. (1982), "The Development of Film in Tanzania" M.A Dissertation, University of Dar es Salaam (Unpublished).

Msokile, M. (1992), *Kunga za Fasihi na Lugha*, EPD, Kibaha.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) (2001), "Kuelekea Kwenye Usawa, Taswira ya Mwanamke Tanzania". Dar es Salaam.

Mulokozi (mh), *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Juzuu *49/2*. Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili,* Dar es Salaam Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Mulokozi, M.M. (1989), *Tanzu za Fasihi Simulizi* Mulika 21:1-2.

Mwakalinga, M.N. (2003), "The Image of Women in Tanzania Films"M.A Dissertation, Universty of Dar es Salaam.

Nabahany, A. (1972), (mh) *Utenzi wa Mwanakupona*. Nairobi, Heinemann.

Njewele, D. C. (2007). "Manifestation of Cultural Performances in Traditional African Films" (Unpublished MA Theatre Arts, Dissertation) University of Dar es Salaam.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi, Jomo Kenyata Foundation.

Noordin, M.M. (2008), "Nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu katika Fasihi ya Kiswahili" katika Ogechi N.O, na wenzake *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Eldoret Kenya, Moi University Press.

Notcutt, L. A. & Lathan, G. C. (1937), *The African and The Cinema*: *An Account of the Work of Bantu Educational Cinema Experment*. London, Edinburgh House.

Nyoni, F.P. (2015) "An Enquiry into Commercial Film Making in Tanzania," *Athetic Value and Prospect*:"Vol.2, No. 1, 70-77.

Omari, S. (2009), "Tanzania Hip Hop Poetry as Popular Literature''(Unpublished Ph.D. Thesis) University of Dar es Salaam.

Pullen, C. (2006), *Marxist against Feminists on Education*. London.

Saadawi, E .(1983), *Woman at Point Zero*. Egypt, Zed Books.

Sen A. (1995), "Gender Inequality and Theories of Justice" katika *Women Cultural and Development: A study of Human Capabilities.* Nussbaum, M c na Jonathan G (Wah). Clarendon Press-Oxford.

Senkoro, F.E.M.K (1987), *Fasihi*. Dar es Salaam, Press and Publicity Centre.

Shule, V. (2004), "Effectiveness of Video Film in Reducing Young Men's Gender Violence and other HIV Risk Behavior", M.A Dissertation, University of Dar es Salaam (Unpublished).

Soko, N. na Senkoro, F.E.M.K. (2009), "Engendered Sports Coverage in Zambia and Tanzania", Paper for Presentation in the Forthcoming CODESRIA Gender Symposium, Cairo.

Sued, A. (2013), "Usawiri wa Ujinsia katika Filamu: Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha katika Filamu za Steven Kanumba." Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria.

Taib A.H. (2008), "Mkabala wa Kiislamu katika Uchanganuzi na Uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili", katika Ogechi N.O na wenzake (wah) *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Eldoret Kenya,* Moi University Press. Uchunguzi wa Kiswahili. Juzuu 64, 53-64.

TUKI, (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: Toleo la Pili. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Universty of Dar-es-Salaam. (Not published).

Wafula, R.M. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Sai Industries Limited,Nairobi.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*, Nairobi.

# VIAMBATISHO

**A: Hojaji Iliyotumika Kukusanyia Data**

1. Je, wewe ni mtazamaji wa filamu za Kibongo?
2. Je, umewahi kutazama filamu yoyote ya Steven Kanumba?
3. Je, mwanamke amesawiriwa vipi katika filamu za Steven Kanumba?
4. Kwa maoni yako, je ni mtazamo gani wa jamii juu mwanamke kupitia filamu teule za Steven Kanumba?
5. Nitajie dhamira chanya na dhamira hasi zinazojitokeza kuhusu mwanamke katika filamu teule za Steven Kanumba.
6. Toa maoni yako kuhusu usawiri wa mwanamke katika filamu za Steven Kanumba.

**B:  Picha Mbalimbali Zinazohusiana na Tasnifu**



Picha namba moja:  Steven Kanumba akiigiza katika mojawapo ya filamu zake (Utafiti 2015).




Picha namba mbili: Jalada la mbele la filamu ya *White Maria* (Utafiti 2015).



Picha namba tatu: Steven Kanumba akiigiza yuko dukani akiwa na Batuli wananunua nguo katika filamu ya *Fake Smile* (Utafiti 2015).



Picha namba nne: Steven Kanumba akiigiza anaumwa na pembeni yuko mkewe Catherine akimtia moyo katika filamu ya *White Maria.* (Utafiti2015)